# Nipashe

Jumamosi Julai 29, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581386

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710

LIKE & FOLLOW US





UKURASA 11

## Serikali yazidi kumkalia kooni Zumaridi

UKURASA 3



## Mchakato wa Katiba Mpya rasmi Septemba

UKURASA 4



Daniel Chongolo | John Mnyika

# Dini na siasa zazua balaa

- **Mkutano** dharura wa vyama waitishwa; CCM, CHADEMA zatwangwa barua... *Uk. 2*

UKURASA 3

## Chalamila azishukia NGO kwa ukiukaji wa maadili





Mwonekano wa mradi wa stendi mpya ya mabasi Mwenge katika Manispaa ya Kinondoni, Dar es Salaam jana, ambapo ujenzi wake unaelekea kukamilika. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## Utata kifo cha Ofisa TRA madai kujirusha ghorofani

UK. 2

**MICHEZO** ROBERTINHO AJIVUNIA FIZIKI WACHEZAJI WAKE UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6



Wafanyabiashara wa pilipili maarufu kama chachandu, wakiwa kwenye lango la stendi ya mabasi ya Kivukoni eneo la Feri, jijini Dar es Salaam jana, wakati wakisubiri wateja wa bidhaa zao. Chupa moja ya chachandu iliuzwa kwa bei ya 1,000/- hadi 2,000/- kulingana na ukubwa wake. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# Dini na siasa zazua balaa

**Na Mwandishi Wetu**

MSAJILI wa Vyama vya Siasa, Jaji Francis Mutungi, amewaita viongozi wa vyama vya siasa nchini katika mkutano wa dharura wiki ijayo, ambao pamoja na mambo mengine, umelenga kuwekana sawa kuhusu ushiriki wa viongozi wa dini katika shughuli za kisiasa.

Amesema, mkutano huo uliopangwa kufanyika jijini Dar es Salaam Jumanne ijayo, unalenga kukumbushana sheria na taaratibu za nchi ili kufanya siasa pasi na kuvuruga umoja wa kitaifa.

Katika mkutano na wahariri wa vyombo vya habari jijini Dar es Salaam jana, Jaji Mutungi alisema kuwa hivi karibuni kumekuwa na hali ya viongozi wa kidini kushiriki katika shughuli za kisiasa kinyume cha taratibu zilizowekwa kisheria, hivyo kutishia mshikamano wa kitaifa. "Lengo si kuzuia watu kushiriki katika siasa kwa sababu ni haki yao, lakini tunahitaji kuwekana sawa kuhusu namna ambavyo wanaweza kushiriki bila kuathiri umoja wa kitaifa," alisema.

Jaji Mutungi alionya kuwa kumekuwa na mambo yanayoibuka miongoni mwa wanasiasa ambayo yasipofanyiwa kazi, yataathiri ustawi wa nchi.

Alisema lengo la mkutano huo ni kutekeleza Sheria ya Vyama vya Siasa, ambayo inaelekeza vyama vya siasa vinapaswa kulinda maslahi ya taifa na mshikamano wa kitaifa badala ya kuwa uwanja wa kueneza mgawanyiko.

"Kuna mambo mengi sana hapa tukiyapuuzia, yatakuja kutupa gharama kubwa katika kuyarekebisha. "Kwa hiyo, pointi yangu kubwa ni kuushusha huo mzigo. Suala la kuchanganya dini na siasa halina afya kwa taifa," Jaji Mutungi alitoa angalizo.

Msajili alitolea mfano, mkutano wa kisiasa wa hivi karibuni mkoani Dar es Salaam wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) uliohusisha viongozi wa dini na kuilazimu ofisi yake kuingilia kati.

Alisema jukumu la msingi la ofisi yake ni kufuatilia utendaji wa vyama vya siasa ili kuhakikisha vinaendesha shughuli zake kwa mujibu wa sheria, ikiwamo Sheria ya Vyama vya Siasa na Sheria ya gharama za Uchaguzi.

"Ni wajibu wetu kufuatilia utendaji wa vyama vya siasa kwa kuwa tuna mamlaka kisheria kusajili na kufuta usajili wa vyama vya siasa," alisema.

Aliwaomba waandishi wa habari kuisadia nchi kuzuia alichokiita wingu kwa kuupa umma habari zinazozingatia maslahi ya taifa na ustawi wa jamii.

Jaji Mutungi pia alionya tabia ya baadhi ya vyama vya siasa kuwavisha sare za chama kingine wafuasi wake na baadaye kufanya vurugu ili kuharibu taswira ya chama kingine.

"Baadhi ya vyama vimekuwa na mchezo wa mambo ya kuwapa wafuasi wao sare za chama kingine. Hii inakwenda sanjari na tulichokuwa tunakataa huko nyuma - kwamba vyama vinakuwa na watu wana kombati za kijeshi kabisa," alionya.

Katika mkutano huo Jesse Kwayu, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Media Brains, alikosoa tabia ya baadhi ya wanasiasa kutumia majukwaa ya makanisa na misikiti "kutoa salamu na kuelezea vitu vyao".

Alikumbusha kuwa Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Nyerere, enzi za uongozi wake, hakwenda kusali msikitini wala kanisani, akiwa amefuatana na waandishi wa habari na baadaye kupewa fursa ya kutoa uamuzi au maagizo ya kiutendaji serikalini.

Naye Mhariri Mwandamizi, Absalom Kibanda, alisema si kosa viongozi wa dini kujihusisha na siasa, kuna mipaka kwao kushiriki shughuli hizo.

"Haitakiwi kutumia nafasi zao kwenye siasa. Tusifanye kama... (alitaja jina la kiongozi wa dini). Anahubiri dini na siasa kwa wakati huohuo," alisema.

Mhariri Mwandamizi wa gazeti la Jamhuri, Jackton Manyerere, alishauri Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa kukemea utaratibu wa walinzi wa viongozi wa kitaifa kuvishwa mavazi ya vyama vya siasa.

**SHERIA**

Katika mkutano huo, Msajili Msaidizi, Sisty Nyahoza, alitoa ufafanuzi wa kisheria kuhusu ushiriki wa viongozi wa dini katika siasa, akisema:

"Katika katiba, ibara ya tatu inasema Tanzania ni nchi ya demokrasia na haina dini isipokuwa watu wana dini. Chama cha siasa hakiwezi kuanzishwa kwa kukiuka sheria za nchi yetu. Sheria inaelekeza kiendeshwe kwa misingi isiyo ya kidini.

"Pia, (chama cha siasa) hakipaswi kuanzishwa kwa kuwagawa watu kwa mrengo wa kidini, maana kitatugawa, utaona sheria inakataza. Hili katazo lipo namna gani na linatekelezwaje huko? "Kiongozi wa dini anaruhusiwa kugombea au asigombee? Tunaamini kwamba kiongozi wa dini yeye binafsi sio kwa cheo chake anaruhusiwa kwenye kuombea nafasi ya kisiasa, lakini sio kwa cheo chake na mavazi yake. "Akienda kwa cheo chake inamaanisha anaunga mkono au kushabikia sera za chama kile. Na inaweza kutafsiriwa kuwa waumini wa taasisi Ile wanashabikia chama fulani.

"Tunashauri viongozi wa dini wasiende kwenye shughuli za kisiasa kunadi sera kwa vyeo vyao na mavazi yao ya taasisi. Waende kama watu binafsi.

"Anaitwa kwenye mkutano wa hadhara, anasema kabisa 'Baba Askofu fulani ni kiongozi wa taasisi fulani'."

Nyahoza pia alitolea ufafanuzi mchakato unaoendelea dhidi ya vyama vipya 18 vilivyoomba kusajiliwa, akisema unaendelea kwa kuzingatia vigezo vya kisheria vinavyojumuisha kuwa na katiba na kanuni, cheti cha kuzaliwa cha watu (wawili) wanaoanzisha chama pamoja na wazazi wako, wawe watazania, walipe ada Sh. milioni moja katika Ofsi ya Msajili wa Vyama vya Siasa, kadi za uanachama, sera za chama zinazotambulika na nembo ya chama.

**VIONGOZI WA DINI**

Shekhe wa Mkoa wa Dodoma, Mustapha Rajabu, alipotafutwa na Nipashe jana kuzungumzia ushiriki wa viongozi wa dini katika siasa, aliwataja viongizi hao ni kama wazazi ambao hawapaswi kuegemea upande wowote.

"Sisi viongizi wa dini vyama vyetu vya kwanza ni dini zetu, lakini siyo kutoka mbele na kuingia katika siasa. Tutakuwa tunajiweka kwenye hatari ya kutokukubalika kwa waumini wetu. Askofu au shekhe hupaswi kutumia majukwaa ya kisiasa kutumika na chama kimoja kukisema kingine," alisema.

Shekhe Rajabu pia alisema ni jambo la aibu kwa kiongozi wa dini kusimama katika jukwaa la kisiasa kukiponda chama fulani.

"Kama unataka kukikosoa chama chochote cha siasa au serikali, unapaswa kutumia mimbari ya kanisani kwako au msikitini kukosoa, siyo mpaka kuropoka mambo ambayo yanaweza kuwagawa waumini wako," alifafanua.

Alisema kuwa kama kuna viongozi wa dini wanataka kujiingiza katika siasa, wanapaswa kujitoa katika dini, vinginevyo wataonekana wavurugaji.

"Viongozi wa dini lazima tujitathmini unakuta Katibu Mkuu wa Taasisi kubwa ya kidini lakini anashiriki katika siasa. Waamini wanatakiwa wangalie na ikibidi wamwondoe katika nafasi hiyo kwani hafai tena kuwa mtumishi wa dini," alishauri.

Canon Mpambichile, Mchungaji Kiongozi wa Kanisa Anglikana Kibaha, mkoani Pwani, aliiambia Nipashe jana kuwa kazi ya viongozi wa dini ni kuombea watu na kushauri, hivyo wanaoingia katika siasa wazingatie ukakasi wake kwa waumini wao.

Shekhe wa Wilaya ya Kibaha, Said Mtonda, alisema viongozi wa dini wanapaswa kujikita katika kutengeneza imani za watu.

Alisema kitendo cha viongozi wa dini kuingia katika siasa ni sehemu ya kufarakanisha waumini kwa kuwa wataona viongozi wao wana mrengo fulani wa chama.

"Unapojiingiza katika siasa wewe kiongozi utaonekana hutoshi," alisema.

Kwa mujibu wa Nyahoza, tangu kuanza usajili wa vyama vingi vya siasa nchini mwaka 1992, vyama 85 vilishashapatiwa usajili wa muda, 25 vikipata usajili kamili, lakini sita vilifutwa kutokana na kushindwa kutimiza masharti ya kisheria, hivyo nchi kuwa na vyama 19 vyenye usajili kamili kwa sasa.

## Utata kifo cha ofisa TRA madai kujirusha ghorofani

**Na Romana Mallya**

MFANYAKAZI wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) Mkoa wa Arusha, Richard Walalaze (35), amekutwa amefariki dunia baada ya kudaiwa kujirusha kutoka ghorofa ya pili ya Hoteli ya Ocean Breeze jijini Tanga.

Hata hivyo kifo hicho kimeibua utata baada ya Jeshi la Polisi kueleza kuwa mwili wa ofisa huyo umekutwa ukiwa na jeraha.

Akizungumza kwa njia ya simu jana, Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Tanga, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Henry Mwaibambe, alimweleza mwandishi wa habari hii kuwa tukio hilo lilitokea jana alfajiri na kwamba mtumishi huyo alikwenda mkoani humo kikazi.

Kamanda Mwaibambe alisema mfanyakazi huyo anadaiwa amejirusha kutoka ghorofa ya pili hotelini hapo alikokuwa amepanga chumba tangu Julai 16, mwaka huu.

"Uchunguzi wa tukio hili unaendelea kufanyika. Leo (jana) alfajiri nilifika eneo la tukio kujionea. Kifo chake kina utata kwani mwili wake una jeraha (bila kutaja eneo la mwili), hivyo tunachunguza.

"Kwa mujibu wa wahudumu wa hoteli, juzi Walalaze alionekana akiongea sana na simu muda mwingi, mara gari lake limegongwa. Tunachunguza kubaini kama ni kweli amejirusha au kuna mengine," alisema Kamanda Mwaibambe.

Alisema taarifa za kuonekana kwa mwili huo hotelini hapo, walizipokea asubuhi ndipo walipokwenda eneo la tukio.

"Nilikwenda nikaona, kuna mambo nimeona wayafanyie kazi kama ni kweli ni kujirusha au kuna mengine," alisema.

## Serikali yazidi kumng'ang'ania Zumaridi

**Na Vitus Audax,**
MWANZA

DIANA Bundala, maarufu kama mfalme Zumaridi mungu chini ya Jua, amefikishwa mahakamani kwa mara nyingine baada ya serikali kutoridhishwa na hukumu aliyopewa ya kifungo cha miezi 12 jela.

Jamhuri imemkatia rufani Zumaridi kutokana na hukumu iliyotolewa Januari 25, mwaka huu, baada ya kumtia hatiani kwa kosa la kuzuia maofisa wa serikali kutekeleza majukumu yao.

Hata hivyo, Zumaridi alitumikia adhabu hiyo kwa kipindi cha mwezi mmoja kutokana na hukumu hiyo kufidia siku alizokaa mahabusu.

Upande wa Jamhuri umepinga adhabu hiyo kuwa ni ndogo kwa mujibu wa sheria na kusajiliwa kwa Namba 32/2023 na kuanza kusikilizwa Julai 27,2023 mbele ya Jaji Cleophace Morris kwa kupokea hoja za rufani hiyo.

Akiwasilisha rufani hiyo, Wakili wa Serikali Mwandamizi, Dorcas Akyoo, akisaidiana na mawakili Frank Nchanila na Adam Murusuli, aliiomba mahakama hiyo kumwongezea adhabu Zumaridi na wenzake wanne kwa madai kuwa adhabu waliyopewa awali ilikuwa ndogo kwa mujibu wa sheria.

Upande wa Zumaridi nao uliwasilisha rufani mahakamani hapo kupinga adhabu hiyo kwa madai kuwa haikustahili kutolewa na imesajiliwa na kupewa namba 72/2023.

Akitoa hoja za rufani hiyo, Wakili wa Zumaridi, Erick Muta aliiambia mahakama hiyo kuwa adhabu waliyopewa wateja wake ilikuwa kubwa kulinganisha na makosa yaliyowatia hatiani.

Alitoa ombi kwa mahakama hiyo kutengua hukumu ya awali ya shauri la jinai namba 10/2022 iliyotolewa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Mwanza chini ya Hakimu Mkazi Mfawidhi Monica Ndyekobora.

Baada ya kusikiliza hoja za pande zote mbili, Jaji Morris aliahirisha shauri hilo na kupanga kulitolea uamuzi Agosti Mosi, mwaka huu, na kueleza kuwa endapo rufani zote zitakubalika zitaendelea kusikilizwa kwa pamoja.




Dereva wa bodaboda akiwa amesheheni madumu matupu ya plastiki katika barabara ya Bagamonyo, eneo la Tegeta mkoani Dar es Salaam mapema wiki hii na kumfanya ashindwe kuona nyuma kitendo ambacho ni hatari kwa usalama barabarani. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Chalamila azishukia NGO ukiukaji maadili

**Na Mary Geofrey**

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila, ameyaonya mashirika yasiyo ya kiserikali nchini kwa baadhi yao kukiuka maadili ya taifa, hivyo kuyataka kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia maadili ya taifa.

Aidha, aliyaonya baadhi mashirika hayo yanayojiingiza kwenye siasa hasa wakati wa kuelekea uchaguzi wa serikali za mitaa na uchaguzi mkuu wa 2025 kwa kuwa kinyume cha taratibu.

Chalamila aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam, wakati akifungua mkutano wa Jukwaa la Mwaka la Mashirika yasiyo ya kiserikali Dar es Salaam (NaCoNGO), lenye kaulimbinu 'Mashirika Yetu, Maadili Yetu, Taifa Letu'.

"Sisi kama taifa tunavyosema maadili kuna vitu vya utamaduni wetu, hivyo taasisi zihakikishe zinafanya kazi kwa kuzingatia maadili yetu. Ni muhimu sana kwa sababu tukiharibu maadili na utamaduni wetu, hatuwezi kujenga taifa letu," alisema.

Chalamila aliwataka wadau wote waliofika katika mkutano huo kuendelea na kazi zao kwa kuzingatia maadili kwa sababu wao ni walalamikiwa wakubwa wa kuvunja na kukiuka maadili ya taifa.

"Kama ulishasoma taifa letu linataka nini ni vyema sasa nawe ukaishi ndani ya maadili ya taifa hili na kila mmoja kutambua mchango wake kwa sababu hakuna mbadala wa taifa lingine ambalo utakimbilia hili likiharibika," alisisitiza.

Aidha, aliwatahadharisha na misaada wanayopokea kutoka kwa wafadhili kujiridhisha kuhusu kuzingatia maadili kwa sababu nyingine ina lenga kuangamiza na si kujenga.

"Niwashauri na vijana ambao mna asasi jiendelezeni kuweni wabunifu, kutafuta miradi inayoleta majawabu ndani ya jamii ili kujisimamia wenyewe na kuepuka kupewa misaada ambayo ina masharti magumu ya kutumaliza," alisema Chalamila.

Kuhusu baadhi ya mashirika kujitumbukiza kwenye siasa, alionya kwa kuyataka kuacha kila sekta kutimiza wajibu wake kwa sababu kuingiliana huko kunaleta mpasuko ndani ya taifa.

"Kama unatoa elimu uraia hakikisha unasimama katika jukumu lako siyo unaingia kwenye chama cha siasa unaanza kuzungumza na kutetea mambo ambayo matokeo yake ni kulivuruga taifa," alisema Chalamika.

Kadhalika aliwasihi vijana wanaomaliza elimu ya vyuo vikuu nchini, kutafuta mbinu mbadala za kujiajiri badala ya kuitupia lawama serikali ilihali imetoa ruzuku ya kupata elimu bure.

"Serikali imejenga majengo ya kisasa ya kusomea lakini anatokea kijana aliyemaliza chuo kikuu anailaumu serikali badala ya kujitafuta na kupambana, imefika hatua sasa wasiyosoma wanawaajiri waliosoma kuwasaidia mambo yao yaendele vizuri.

"Siyo ajira za serikali zinatolewa kwa undugu, mimi nina ndugu gani aliyenitetea nikawa hapa, angalieni vijana wanauza vitu kariakoo, wametoka vijijini sasa waaminiwa hadi na benki na kukopeshwa mamilioni ya fedha lakini wasomi na walioajiriwa hawawezi kuaminiwa kukopeshwa kiasi kikubwa," alisema.

Naye Mwenyekiti wa NaCoNGO Mkoa wa Dar es Salaam, Jane Magigita, alisema mkutano huo unalenga kutoa elimu kwa jamii na mashirika nchini.

Alisema pia wanatoa elimu mbalimbali ikiwamo ya fedha na sheria ya kodi kwa wanachama hao, nakumwomba Chalamila kuhimiza kutengwa kwa bajeti ya mkoa kwa ajili ya kusaidia vijana.

Magigita alilalamikia mashirika hayo kutozwa kodi kubwa na kuhudumiwa kama kampuni jambo linalofanya kushindwa kutoa huduma kikamilifu.

Chalamila aliahidi serikali itafanyia kazi jambo hilo kwa kuzikutanisha taasisi hizo na wanaobadili sheria waikiwamo Bunge, Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na wadau wengine ili kupitia upya sheria hiyo ya kodi.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe:@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Mtumba,
S.L.P. 2888,
DODOMA,
29.07.2023

**TAARIFA KWA UMMA**

1. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta ya Ujenzi) inapenda kuutaarifu umma kuwa siku ya Jumanne tarehe **01-08-2023** kampuni ya **Mainline Carriers Ltd** itasafirisha Mizigo yenye vipimo vikubwa kutoka **Dar-Es-Salaam Port** kuelekea **JNHPP SITE**, gari hizo zina namba za usajili: T 624 DFA / T 568 EAZ, T 868 DDC / T 881 EAU, T 167 DFC / T 310 DDH, T 778 EAP / T 387 DHQ, T 970 DTN / T 321 DDH

2. Gari hizo zina vipimo vifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| **Urefu** | - | **mita 19.80** |
| **Upana** | - | **mita 7.40** |
| **Kimo** | - | **mita 4.60** |

2. Njia itakayotumika: **BANDARI YA DAR ES SALAAM hadi JNHPP SITE** kupitia **KILWA ROAD, KIBITI, MLOKA.** Gari zitasafiri muda wa usiku ***(Kuanzia saa 06:00 Usiku mpaka saa 11:00 Alfajiri)*** Kutoka **Dar es Salaam Port mpaka Bungu.**
Kutoka **Bungu kwenda JNHPP** Site gari zitasafiri muda wa mchana ***(kuanzia 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)***

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.**

# Mchakato Katiba Mpya rasmi Septemba

**Na Ibrahim Joseph,**
SONGEA

SERIKALI imesema inatarajia kuanza rasmi mchakato wa Katiba Mpya Septemba, mwaka huu, kwa makundi maalumu kuanza kutoa elimu ya katiba.

Makundi hayo ni pamoja na wasomi wa vyuo vikuu, viongozi wa madhehebu ya dini pamoja na sekta binafsi.

Akizungumza na waandishi wa habari juzi mjini hapa, Waziri wa Katiba na Sheria, Dk. Damas Ndumbaro, alitaja kundi lingine kuwa ni waandishi wa habari kuandika na kutangaza ili umma ujue maendeleo ya mchakato huo.

Waziri huyo alisema mchakato huo wa Katiba Mpya unatarajia kuanza kwa kushirikisha makundi hayo kuelimisha umma kuhusu katiba.

Alibainisha kuwa lengo la kuanza utoaji wa elimu ni kuhakikisha kila Mtanzania anajua vizuri Katiba iliyopo na kujua uzuri wake na upungufu ili kufanya marekebisho.

"Na sisi hatusemi Katiba iliyopo haina mapungufu la! Ndiyo maana tunasema yale mazuri tuyabainishe kwamba jamani hili ni zuri, hasa kama ni nzuri kwa nini tuliondoe. Basi kama litakuwa zuri tutasema liendelee kuwapo kwenye Katiba Mpya, lakini likiwa baya tutasema tuachane nalo," alisema.

"Serikali imejipambanua lazima iwapatie wananchi wa Tanzania Katiba Mpya na bora zaidi kuliko Katiba yoyote ambayo imewahi kutokea hapa nchini. Kwa hiyo ni dhamira ya serikali kuwapatia wananchi Katiba hiyo mpya," alisisitiza.

Dk. Ndumbaro alisema utoaji wa elimu utasaidia kila mtu kuisoma na kuchambua yaliyomo kwenye Katiba ya sasa kwa sababu hawawezi kuchambua kitu wasichokijua.

Pia alisema, kuna asilimia chache ya Watanzania wanaojua Katiba iliyopo, hivyo wanahitaji elimu ya kushirikishwa kabla ya kutoa maoni yao kuhusu katiba mpya.

Alisema hatua za awali zimeanza kwa serikali kutenga fedha kwenye bajeti ya mwaka 2023/24 iliyopitishwa na Bunge kwenye kipengele kidogo cha Katiba na ziliongezwa kwa zaidi ya asilimia 180.

Ndumbaro aliongeza kuwa kwa kuanzia Bunge limepitisha Sh. bilioni tisa kwa ajili kuanza kwa mchakato wa Katiba Mpya ambazo hazitoshi, hivyo wanakusudia kuomba bajeti ndogo Desemba, mwaka huu, kwa ajili ya mchakato huo.



Makamu Mwenyetiki wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Kanali mstaafu Abdulrahman Kinana (kulia), akifurahia jambo na baadhi ya waganga wa tiba mbadala, baada ya kuwasili wilayani Itilima mkoani Simiyu jana na kufanya mazungumzo nao. **PICHA MAULID MMBAGA**

# Petroli yaadimika Tanga, bei juu, EWURA yanena

**Na Steven William,** MUHEZA

WAKATI Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) ikitangaza kushuka kwa bei za mafuta, katika hali isiyo ya kawaida, wananchi wilayani Muheza mkoani Tanga wamekumbwa na adha ya ukosefu wa nishati hiyo, hasa petroli.

Hali hiyo imetajwa kuchangia ongezeko la gharama za usafiri kwa abiria wanaotumia usafiri wa umma.

Meneja wa EWURA Kanda ya Kaskazini, Lorivii Long'idu, alimwambia mwandishi wa habari hii jana kuwa, mafuta yapo lakini tatizo kubwa ni baadhi ya wafanyabiashara kutokuwa na mkataba na kampuni kubwa zinazoagiza mafuta kutoka nje kuja Tanzania.

Mwandishi ameshuhudia katika kituo cha mafuta cha Mnyamuru kukiwa na foleni kubwa ya magari pamoja na pikipiki huku madereva wakiambiwa tulimaliza mafuta tangu juzi.

Mpaka jana, vituo vyote vitano vya kuuzia mafuta vilivyoko wilayani hapa ambavyo ni Mvuleni, COPEC, BP, Mnyamuru na Mikwamba vilikuwa havitoi huduma huku sababu zikielezwa na wamiliki wa vituo kuwa mafuta yameisha.

Mmoja wa wamiliki wa vituo hivyo vya kuuzia mafuta wilayani Muheza ambaye aliomba jina lake lihifadhiwe, alisema wanatarajia kupata mafuta kuanzia mwezi ujao.

Dereva wa pikipiki ya miguu mitatu, yaani Bajaji, Juma Rajabu, alisema ukosefu wa mafuta umesababisha baadhi yao kuishiwa nishati hiyo wakiwa safarini.

Alisema hali hiyo imesababisha mafuta ya petroli kupanda bei kutoka Sh. 2,700 mpaka Sh. 4,000 kwa lita.

UFAFANUZI EWURA

Katika ufafanuzi wake, Long'idu alisema wanapokuwa na mkataba na kampuni kubwa wanakuwa wanatambulika na kampuni hizo kwamba wana wateja wangapi Muheza, hivyo wanapelekewa mafuta kulingana na idadi wanayotaka.

Meneja huyo alisema wamiliki wa vituo wanataka wafanye biashara kwa kuhakikisha wanaingia mkataba na kampuni kubwa zinazoagiza mafuta nje na tayari wameshaanza kufanya hivyo na baadhi ya wamiliki wa vituo vya mafuta wanapata mafuta.

# Mkunda: Majenerali waliostaafu bado hazina

**Na Mwandishi Wetu**

MKUU wa Majeshi ya Ulinzi Tanzania, Jenerali Jacob Mkunda, amesema majenerali sita waliostaafu akiwamo Meja Jenerali Antony Sibuti, bado ni Jeshi la Akiba na kwamba wakati wowote watakapohitajika, wataitwa kwenda kulitumikia Jeshi hilo kama Wanajeshi wengine ndani ya miaka mitatu.

Alisema Majenerali hao bado wanahesabika ni sehemu ya Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) kwa kipindi cha miaka mitatu kuanzia jana walipoagwa kwa mujibu wa utaratibu wa Majenerali kusukumwa wakiwa kwenye Magari Maalumu na Maofisa wenzao walioko kazini.

"Majenerali tuna Utamaduni na Utaratibu wetu wa kuagana wakati wa kustaafu. Hawa bado ni sehemu ya sisi, ni Jeshi la Akiba. Tukiwahitaji ndani ya miaka mitatu ijayo wanakuja wanalitumikia Jeshi kama Wanajeshi wengine. Nimepokea vitambulisho vyao vya kazi hapa na mimi nimewakabidhi vitambulisho vya kustaafu," alisema Jenerali Mkunda.

Awali, taarifa ya jeshi hilo, ilisema Meja Jenerali Sibuti (61), aliajiriwa na JWTZ Julai Mosi, 1987 na amelitumikia kwa miaka 35 na siku 24 mpaka alipostaafu Desemba 28, mwaka jana.

Wengine ni Brigedia Jenerali Egbert Kambanga (60), amelitumikia jeshi kwa miaka 34 na miezi saba, Brigedia Jenerali Peter Gaganija (60), amelitumikia jeshi kwa miaka 38 na siku 21.

Brigedia Jenerali Adolph Muta (60), amelitumikia jeshi kwa miaka 35 na miezi 10 na siku 14, Brigedia Jenerali Abdallah Alfonce (60) miaka 38 na miezi sita na Brigedia Jenerali Julius Mbwelo (60), amelitumikia miaka 38 na miezi sita.

Akizungumza kwa niaba ya wastaafu wenzake, Brigedia Jenerali Muta alisema anamshukuru Mungu kwa kuwafikisha katika siku hiyo muhimu ya utumishi na kwamba kwa sasa bado wao ni Jeshi la Akiba na wakati wowote watakapohitajika, watarudi kulitumikia Taifa.

Alisema kazi ya Jeshi si wajibu, bali ni wito na kuwa tayari kujifunza kutoka kwa wakubwa na wadogo kwa kuwa JWTZ inaheshimika kwa sababu ya utii.

Majenerali hao waliagwa jana kwa mujibu wa utaratibu na utamaduni wao katika Kambi ya Jenerali Twalipo, Mgulani, Dar es Salaam.



Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Shinyanga, Leonard Nyandahu, akionesha kwa waandishi wa habari mkoani humo mapema wiki hii, matairi matano ya lori yaliyoibwa kwenye ujenzi wa reli ya kisasa (SGR). **PICHA: MARCO MADUHU**

# Mwigulu ataka kasi upatikanaji wa mkandarasi daraja Mto Msimbazi

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba, ameitaka Wakala wa Barabara (TANROADS) kukamilisha mchakato wa upatikanaji wa Mkandarasi atakayejenga Daraja la Mto Msimbazi ili kuwaondolea wakazi wa Jiji la Dar es Salaam, changamoto ya mafuriko.

Dk. Nchemba alisema hayo jana baada ya kuongoza ujumbe wa serikali na Benki ya Dunia kutembelea eneo la Jangwani ambako mradi wa uendelezaji wa Bonde la Mto Msimbazi unatarajiwa kutekelezwa ikiwemo ujenzi wa daraja kubwa la juu la Jangwani, kwa ufadhili benki hiyo mapema mwakani, kwa gharama ya zaidi ya Dola za Marekani milioni 350.

"Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan ametuelekeza tufanye kikao na Benki ya Dunia ili mradi huu wa daraja na ujenzi wa barabara za Jiji la Dar es Salaam, uanze kutekelezwa haraka ili kuwaondolea wakazi wa jiji la Dar es Salaam kero ya mafuriko pamoja na kuimarisha mipango miji," alisema.

Dk. Nchemba alisema kuwa Jiji la Dar es Salaam ni kitovu cha biashara na linategemewa na nchi karibu zinazopakana na Tanzania na kwamba kukamilika kwa miradi hiyo ya daraja na barabara za jiji kutachochea shughuli za kiuchumi.

"Wizara ya Fedha kupitia Benki ya Dunia tunawahakikishia kuwa fedha zipo kinachotakiwa ni kuanza kwa utekelezaji ili kutekeleza maelekezo ya Rais," alisisitiza.

Naibu Waziri wa Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Deo Ndejembi, ambao ndio watekelezaji wa mradi huo, aliahidi kusimamia utekelezaji wa mradi huo kwa ufanisi ili thamani ya fedha itakayotumika ilingane na ubora wa mradi.

Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila, alihimiza pia kuanza haraka kwa ujenzi wa mradi huo ili kutatua kero za wananchi wa Dar es Salaam na kuzingatia usanifu wa viwango vya juu.

"Ujenzi wa barabara na madaraja makubwa kama haya kuna maanisha kuufungua mkoa kiuchumi sasa tusibaki kulumbana na kubishana kwa ajenda ndogo ambazo wakati fulani hazina mashiko kwa mustakabali wa taifa letu. Lakini pia ile maana halisi ya mkoa wa Dar es Salaam kuwa Jiji la kibiashara ionekane kwa miundombinu hii" alisema.

Mwakilishi Mkazi wa Benki ya Dunia, Nathan Belete, alisema benki yake itatoa mkopo nafuu wa dola za Marekani milioni 350 ili miradi hiyo itakayotekelezwa jijini Dar es Salaam ichangie maendeleo ya nchi kwa kupanga mji, kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, kuboresha miundombinu ya usafiri na kudhibiti taka ngumu.

Baadhi ya wakazi wa Dar es Salaam wamekuwa wakipoteza muda na mali zao wakati wa mafuriko na kwamba ujenzi wa daraja hilo kubwa na refu litakaloanzia Magomeni hadi Fire, utakuwa mwarobaini wa matatizo yao.

Mradi wa Uendelezaji wa Bonde la Mto Msimbazi (DMDP II) utatumia fedha hizo za serikali na mkopo kutoka Benki ya Dunia kujenga miundombinu ya barabara, mifereji, maeneo ya wazi, masoko, vituo vya mabasi, na kurekebisha miundombinu ya taka ngumu, miundombinu ya usafiri, mabadiliko ya tabianchi kwa jiji la Dar es Salaam zinazosababisha mafuriko na kudhibiti taka ngumu.

# TCAA yazungumzia 'ajali ya ndege' Mkuranga

**Na Joseph Mwendapole**

MAMLAKA ya Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA), imesema ajali ya ndege aina ya Embraer 120, inayodaiwa kuanguka katika kijiji cha Msufini Kidete, Mkuranga mkoani Pwani ilikuwa ya kupima utayari wa ukoaji.

Ndege hiyo inadaiwa kuanguka ikitokea uwanja wa Kilwa Masoko mkoani Lindi Kwenda Tanga ikiwa imebeba abiria 25.

Meneja Uhusiano na Mawasiliano wa TCAA, Yessaya Mwakifulefule, aliwaambia waandishi wa habari jana kwamba kilichofanyika ilikuwa kupima uwezo na utayari wa nchi wa kukabiliana na matukio ya utafutaji na uokoaji wa ndege zinazopata ajali kwenye nchi kavu au majini.

Alisema zoezi hilo liliandaliwa (TCAA) ambayo ina jukumu la kuratibu na kusimamia huduma ya utafutaji na uokoaji wa ndege zinazopata ajali kwenye anga la Tanzania.

TCAA, ilisema imeshirikiana na taasisi za udhibiti wa usafiri wa majini ambazo ni Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC) kwa Tanzania Bara na Mamlaka ya Usafiri wa Baharini (ZMA) kwa upande wa Zanzibar.

"Zoezi hili pia limehusisha taasisi za utafutaji na uokoaji za umma na binafsi kama Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), Jeshi la Polisi, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA), mashirika ya ndege, mashirika ya vyombo vya majini, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania (TAA), Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA), hospitali, Shirika la Msalaba Mwekundu Tanzania (Red Cross), wavuvi na wadau wengine mtambuka wa utafutaji na uokoaji," alisema.

Alisema Tanzania iliridhia Mkataba wa Kimataifa wa Usafiri wa Anga (ICAO) mwaka 1962 na Mkataba wa Shirika la Bahari Duniani (IMO) mwaka 1974 na kuwa mwanachama wa mashirika hayo.

Mikataba hiyo yote inayosimamiwa na ICAO na IMO, alisema inazitaka nchi wanachama kutoa huduma za utafutaji na uokoaji katika usafiri wa anga na majini wakati ajali na matukio ya dharura ya vyombo vya usafiri wa anga na majini ndani ya eneo la nchi mwanachama.

# TANESCO, Gridworks zatiliana saini ujenzi njia umeme mikoa ya kaskazini

**Na Faustine Feliciane**

SHIRIKA Umeme Tanzania (TANESCO) limeingia makubaliano ya awali (MoU) na kampuni za Gridworks Development Partners LLP ya Uingereza na Larsen &Turbo Ltd ya India kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya kusafirishia umeme kutoka Chalinze kwenda mikoa ya Tanga na Arusha.

Kampuni hizo zilitia saini makubaliano hayo jijini Dare s Salaam juzi na ujenzi huo utafanyika kwa miezi 30 mpaka kukamilika kwake.

Akizungumza katika hafla hiyo, Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO, Maharage Chande, alisema mradi huo wa miundombinu ya kusafirishia umeme, utaondoa kero ya kukosekana umeme mara kwa mara katika mikoa hiyo kutokana na njia hiyo kuzidiwa.

Chande alisema mahitaji ya umeme katika mikoa ya Arusha, Tanga na Kilimanjaro yameongezeka zaidi kutokana na kuwapo kwa viwanda, hivyo kusababisha njia kuzidiwa kutokana na mahitaji ya umeme katika mikoa hiyo.

"Ujenzi wa miundombinu ya njia hii sasa utapekea mikoa hii kupata umeme kwa uhakika na kuharakisha shughuli za maendeleo katika maeneo hayo," alisema Chande.

Alisema kwa mara ya kwanza wameruhusu sekta binafsi kuwekeza katika mradi huo kwa kuwa wameona maendeleo yake kwa nchi zingine. Chande alisema kupitia makubaliano yao, kampuni hizo zitajenga miundombinu hiyo kwa gharama zao na TANESCO italipa taratibu baada ya mradi kukamilika.

"Tutakachokifanya tutaunda tume ya pamoja kati yetu TANESCO na wenzetu hawa. Kazi ya kwanza itakuwa utayarishaji wa mradi na kutakuwa na kazi ya kuipitia upya njia iliyopo sasa na kuangalia hali yake ilivyo na baada ya hapo, kazi ya pili itakuwa utekelezaji wa mradi wenyewe," alisema.

Chande alisema mradi huo utachukua miezi minane hadi 12 kwenye utayarishaji wake na miezi 18 kwenye utekelezaji wake. Alisema wakati wa utayarishaji wa mradi watajua thamani kamili ya mradi.

"Katika kamati itakayoundwa kwa pamoja tutafanya tathmini tujaua thamani ya mradi, japo gharama ya ujenzi itakuwa ya hizi kampuni, na sisi baadae tutaanza kulipa lakini tutakuwa tumejua thamani halisi tutakayotakiwa kulipa," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa Gridworks, Simon Hodson, alisema kampuni hiyo ina uzoefu mkubwa wa ujenzi wa njia za kusafirishia umeme na itatekeleza mradi huo kulingana na makubaliano.

Alisema wanafahamu umuhimu wa kuwa na njia imara za kusafirishia umeme na mradi utakapokamilika utasaidia kuongeza kasi ya maendeleo.

Kampuni hiyo ambayo iko chini ya serikali ya Uingereza, itafanya kazi kwa pamoja na kampuni ya ujenzi ya Larsen &Turbo Limited na Makamu wa Rais na Mkuu wa kampuni hiyo Kanda ya Afrika, Rahul Sikka, alisema wana uzoefu mkubwa na Tanzania na wanaamini mradi huo utakamilishwa kwa wakati na kwa kiwango cha juu.

Alisema kampuni yake imeshafanya kazi nchini na kwa sasa inatekeleza na mradi wa ujenzi wa njia za umeme kwenye Reli ya Kisasa (SGR).

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Tunazikumbusha timu zetu hakuna kibonde mashindano ya CAF

**WIKI** hii Shirikisho la Soka Afrika, CAF, lilichezesha droo ya michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika na Kombe la Shirikisho kujua timu shiriki zitakutana na mpinzani gani kuanzia hatua ya awali ya michuano hiyo.

Katika droo hiyo zipo timu ambazo zitaanzia hatua ya awali kabisa na zipo timu nyingine kutokana na mafanikio yao kwenye michuano hiyo ndani ya miaka mitano ya karibuni zimepangwa zianzie hatua ya kwanza.

Kwa msimu huu wa 2023/2024 Tanzania Bara kwa mara nyingine itawakilishwa na timu nne, mbili katika kila mashindano ambapo Simba na Yanga zitashiriki Ligi ya Mabingwa wakati Azam FC na Singida Fountain Gate zenyewe zitashiriki kombe la Shirikisho Afrika.

Kati ya wawakilishi wetu hao wote, ni Simba pekee ndiyo itakayoanzia raundi ya kwanza ikisubiri timu itakayovuka hatua ya awali kati ya Africans Stars ya Namibia itakayocheza na Power Dynamos ya Zambia.

Yanga imeshafahamu itakutana na Asas ya Djibouti kwenye hatua ya awali, Azam itacheza na Bahir Dar Kanema ya Ethiopia na Singida FG yenyewe inafahamu itacheza na ndugu zao wa JKU ya Zanzibar.

Siku chache baada ya kuchezeshwa kwa droo hiyo na kupangwa ratiba kamili, tayari hapa nchini kumeibuka maneno miongoni mwa mashabiki wa timu hizo wengi hususani wa klabu za Simba na Yanga zikijisifia kupangiwa na timu 'vibonde' kwenye michuano hiyo.

Mashabiki hao wameenda mbali kwa kusema wapinzani wa timu hizo hawana majina makubwa katika soka la Afrika kama zilivyo klabu zao.

Tunazikumbusha klabu zetu kwenye mashindano haya ya CAF hususani kwenye hatua hizi za mchujo kunakuwa na matokeo ya kushangaza zaidi kwa timu kubwa.

Inawezekana timu watakazocheza nazo hazina majina makubwa Afrika, lakini hiyo si sababu ya kuzidharau kwa sababu kama watakavyokuwa wao uwanjani na wachezaji 11 ndivyo na wapinzani wao watakavyokuwa uwanjani na idadi hiyo ya wachezaji.

Tunazikumbusha klabu zetu kutoingia uwanjani na matokeo yao mfukoni badala yake wajipange na kujiandaa vizuri kukabiliana na wapinzani wao hao.

Mpira ni mchezo wa makosa, kama klabu zetu hazitakuwa makini na kufanya makosa uwanjani zitajikuta zikitupwa nje ya mashindano mapema na kushindwa kufikia malengo yao kwenye michuano hiyo msimu huu. Hali hii ya kutolewa mapema kwenye hatua ya awali haitakuwa habari mpya kwa klabu zetu, ikumbukwe katika miaka ya karibuni, mwaka 2019 Simba ikiwa imetoka kutinga hatua ya robo fainali msimu wa nyuma yake ilijikuta ikitolewa kwenye mashindano ya klabu bingwa kwa kushangazwa na klabu ya UD Songo ya Msumbiji ambayo hapo kabla ilikuwa haifahamiki hapa nchini.

Kama hiyo haitoshi, msimu wa mwaka 2021, Simba kwa mara nyingine ikiwa imetoka kwenye hatua ya robo fainali msimu uliotangulia ilijikuta ikitupwa nje na Jwaneng Galaxy ya Botswana ikiwa haitambuliki hapa nchini.

Hii ni mifano michache ya kuashira mpira ni mchezo wenye matokeo ya kushangaza, hivyo ni lazima wawakilishi wetu wote kujiandaa vizuri na kuacha kudharau wapinzani wao bila kujali zinatoka katika ukanda gani wa soka hapa Afrika.


Tunaamini kama wawakilishi wetu watajiandaa vizuri na kuwa na nidhamu ya mpira wanaweza wakasonga mbele kuelekea kwenye malengo yao kwenye michuano hiyo ya Kimataifa inayoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika yaani CAF.

Tunazitakia kila la heri klabu zote ambazo zitaiwakilisha nchi kwenye michuano hiyo ya kimataifa, mashabiki wao wana matumaini makubwa na klabu zao hivyo wasiwaangushe, lakini pia kufanya kwao vizuri ni heshima na sifa kwa Taifa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:**
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Siasa za Simba, Yanga nje ya uwanja zisiumize watu vichwa

Na Adam Fungamwango

**HIVI** karibuni klabu ya Simba ilimuacha kiungo wake aliyeitumikia klabu hiyo kwa miaka 13, Jonas Mkude na baada ya siku chache tu akasajiliwa na mahasimu wao wa jadi Yanga.

Kabla ya kusajiliwa tuliwasikia viongozi wa klabu ya Simba wakisema watamuaga mchezaji wao huyo kwa gwaride la heshima siku ya tamasha la Simba Day na wakaenda mbali zaidi kusema wataistaafisha jezi namba 20 ambayo aliichezea kwa miaka yote hiyo.

Kwa mujibu wa Meneja Habari na Mawasiliano wa Klabu hiyo, Ahmed Ally, alisema kuwa jezi namba hiyo atakuja kupewa mchezaji kutoka kikosi cha pili ambaye ataonekana anafanya vyema.

Baada ya kusajiliwa na Yanga, baadhi ya vyombo vya habari vilitaka kusikia kauli ya viongozi wa Simba kama watamuaga mchezaji huyo kwa gwaride la heshima kama walivyodai awali au lah.

Niliwasikia viongozi wa wawili wa Simba, Ofisa Mtendaji Mkuu, Imani Kajula na hata Ahmed wakisema lengo lipo pale pale, kumuaga Mkude kwa heshima licha ya kwamba amejiunga na watani zao wa jadi, Yanga.

Wakasema wala haiwapi shida kwa sababu mchezaji wao kuhamia Yanga kwa kuwa yupo kazini, haijalishi ni kwenye klabu ya Yanga, hivyo watamuaga tu.

Picha likaanza pale Mkude alipotambulishwa rasmi kwa mbwembwe kwenye klabu yake mpya. Kwanza kabisa akaibusu nembo ya Yanga halafu kwenye ukurasa rasmi wa klabu kilitengenezwa kikatuni ambacho kilionyesha mchezaji huyo anamkata kichwa mnyama Simba.

Kuna baadhi ya watangazaji wa michezo na wachambuzi wakawa kama hawakupendezewa na kitendo kile walichokiita si cha kiungwana.

Binafsi nikacheka kwani mimi nazifahamu klabu hizi kubwa mbili uhasimu wao na utani wa jadi.

Tangu miaka ya nyuma kumekuwa na matukio mbalimbali ambayo afadhali hata haya.

Mengi sitaki kuyaainisha hapa kwa sababu za kimaadili, lakini haya ndiyo maisha ya klabu hizo nje ya Uwanja na siasa zake.

Klabu hizi zinakuwa na matukio ya utani na siasa mbalimbali ya kiungwana na yasiyo ya kiungwana kwa pande zote mbili, hadi leo hakuna chochote kinachoweza kuzuia hilo, labda tu wafanye matukio ya kuvunja sheria za nchi.

Haya ndiyo maisha yao na wataendelea kuwa nayo, watangazaji wa michezo na wachambuzi wanaweza kuumia vichwa tu wakiyafuatilia na kuyapa kipaumbele sana kwenye vipindi vyao kuliko soka lenyewe la uwanjani.

Tukirudi kwenye suala la Mkude ni kwamba, Ofisa Habari wa Yanga akajitokeza na kusema hawawezi kukubali Mkude kwenda kuagwa siku ya Simba Day, labda wao Simba ndiyo wangeenda kumuaga siku ya Tamasha la Mwananchi.

Hapa ina maana Yanga imekataa, mchezaji wao hawezi tena kuagwa na wapinzani wao Simba.

Hii nayo pia ikawapa tabu watangazaji na wachambuzi wakitumia muda mwingi kuliongelea kuliko hata mambo ya usajili na maandalizi ya msimu.

Kwetu sisi wengine wala hatukushangaa, ni zile zile siasa za Simba na Yanga nje ya uwanja, hivyo ya 'Ngoswe tulimuachia Ngoswe.'

Juzi mchezaji Che Fondon Malone alionekana amevaa jezi namba 20 ambayo klabu ya Simba ilidai kustaafisha, ukawa mjadala ambao hauna tija kwa sababu binafsi niliamini kabisa baada ya kutokea kutoelewana kati ya viongozi wa timu hizo mbili, basi kila kitu kitakuwa kimekufa.

Ahmed akatolea ufafanuzi ulioonekana ni wa 'kiuandamizi' zaidi, akidai alipewa Ahmed Feruzi, golikipa aliyepandishwa kutoka kikosi cha pili ambaye naye aliamua kumpaa mchezaji huyo ambaye ni beki mpya aliyesajiliwa kutoka Coton sport ya Cameroon.

Kifupi hapa ni kwamba baada ya Mkude kufanya vitu vilivyoonekana kuikera Simba, huku Yanga ikikataa asiende kuagwa, sidhani kama nayo ingekubali kuendelea kuistaafisha namba hiyo.

HABARI KITAIFA

# Bilioni 68/- kutumika ujenzi miundombinu mipya ARU

**Na Joseph Mwendapole**

CHUO Kikuu Ardhi (ARU) kimeingia mkataba wa ujenzi wa majengo mapya manne ya chuo hicho na Kampuni ya Kimataifa ya Jiangxi kwa gharama ya Sh. bilioni 67.7.

Ujenzi huo utakaohusisha pia maabara mtambuka yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 670, utakiwezesha chuo kuongeza udahili wa wanafunzi kutoka 6,074 kwa sasa hadi kufikia 12,620.

Mkataba huo ulitiwa saini jana chuoni huko baina na Makamu Mkuu wa (ARU), Prof. Evaristo Liwa na Mkurugenzi wa Kampuni ya China Jiangxi International Economic and Technical Cooperation Co. Ltd, Peng Chao. Mkataba wa ujenzi huo unatokana na mradi wa upanuzi wa vyuo vikuu uitwao Higher Education for Economic Transformation (HEET) unaotekelezwa katika vyuo vya umma 14, taasisi tatu za elimu ya juu na vyuo vitano ambavyo viko chini ya Wizara ya Fedha na Mipango. Baada ya kutia saini mkataba huo, Prof. Liwa alisema mradi huo ni wa miaka mitano na unafadhiliwa na Benki ya Dunia (WB) na unaratibiwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

"Sisi (ARU) ni wanufaika wa mradi huu. Tulipata Dola za Marekani milioni 29 ambazo ni sawa na Sh. bilioni 67.7. Mradi huu unalenga kukijengea uwezo chuo chetu katika mambo mbalimbali ikiwamo kuongeza kiwango cha udahili wa wanafunzi na kuboresha mitaala ya kufundishia ili kuendana na mahitaji ya soko hususan katika programu za kipaumbele za mradi," alisema.

Alisema mradi huo pia utasaidia vyuo mbalimbali nchini kuboresha utawala bora katika sekta ya elimu ya juu na kutaja maeneo ambayo chuo hicho kimejikita kutekeleza mradi huo kuwa ni pamoja na ujenzi na uboreshaji wa miundombinu na kuhuisha mitaala ya kufundishia.

Alitaja eneo lingine ni kufanya utafiti unaolenga kutatua matatizo ya jamii kwa kuzingatia ubunifu na uvumbuzi katika utafiti na kujenga uhusiano wenye tija baina ya chuo hicho na vyuo vingine na sekta binafsi. Alisema kupitia mradi huo, wataanzisha mafunzo kwa njia ya mtandao kwa kutumia teknolojia ya kisasa na kukiwezesha chuo kuwa na miundombinu na vifaa bora vya kisasa vya mawasiliano kwa kutumia teknolojia ya kompyuta.

Prof. Liwa alisema eneo lingine ambalo watafanya maboresho kupitia mradi huo ni kujenga uwezo wa wanataaluma wa ARU na uwezo wa kiuongozi.

Alisema majengo yatakayojengwa ni madarasa yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 4,604 na maabara mtambuka yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 670 kwa wakati mmoja.

Alisema, majengo hayo yatakuwa na studio zenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 780 na karakana za ufundi majengo zenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 492.

"Majengo yote kwa ujumla yatakuwa na uwezo wa kuchukua wanafunzi 6,546 na walimu 93 kwa mkupuo, ujenzi huu utakiwezesha chuo kuongeza udahili wa wanafunzi kutoka 6,074 kwa sasa hadi kufikia 12,620 ambao unaendana na matokeo ya mpango wa chuo wa miaka 10," alisema Prof. Liwa.




Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu Ardhi (ARU), Prof. Evaristo Liwa (kulia), akibadilishana nyaraka na Mkurugenzi wa Kampuni ya China Jiangxi International Economic and Technical Cooperation Ltd, Peng Chao, baada ya kutiliana saini mkataba wa ujenzi wa majengo mapya ya chuo hicho kampasi kuu ya Dar es Salaam juzi. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Maofisa elimu wasisitizwa usimamizi ujenzi madarasa

**Na Steven William, MUHEZA**

KAMATI ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya ya Muheza, imewaagiza Maofisa Elimu wa msingi na sekondari na wa kata katika Halmashauri ya Wilaya ya Muheza kusimamia elimu na ujenzi wa miradi usiku na mchana.

Lengo la kufanya hivyo ni kuhakikisha miradi hiyo inakamilika kwa kuwawezesha wanafunzi wa kidato cha tano kupata miundombinu bora ya elimu.

Agizo hilo limetolewa jana baada ya kamati hiyo, ikiongozwa na Katibu Tawala wa wilaya hiyo, Mohamed Mfaki, kufanya ziara ya kukagua miradi ya ujenzi wa vyumba vya madarasa katika Shule ya Sekondari ya Muheza.

"Tumtie nguvu Rais wetu, Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa kusimamia utekelezaji wa miradi hii usiku na mchana na kuhakikisha inakamilika ili wanafunzi wa kidato cha tano watakaoripoti wawe na miundombinu ya kutosha kulingana na idadi yao," alisema.

Mfaki aliwataka maofisa elimu kufuata taratibu zilizobainishwa katika kusimamia ipasavyo shughuli zote za elimu ikiwamo ujenzi wa shule mpya na miundombinu inayojengwa katika maeneo yao.

Alisema ofisi yake haitamfumbia macho yeyote atakayeshindwa kusimamia na kukamilisha miradi hiyo kwa kuwa atakuwa ameshindwa kutekeleza wajibu wake kikamilifu.

Pia, aliwataka maofisa elimu kufuata taratibu zilizobainishwa katika kusimamia shughuli zote za elimu ikiwamo ujenzi wa shule mpya na miundombinu.

Mkuu wa Shule ya Sekondari ya Muheza, Boniface Kinyemi, alisema serikali imetoa Sh. milioni 464 kwa ajili ya ujenzi wa mabweni mawili, vyumba vya madarasa saba na matundu ya vyoo 14 katika shule hiyo yenye kidato cha tano na sita.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, Dk. Jumaa Mhina, alisema walimu wakuu wa shule za msingi na wakuu wa shule za sekondari na waratibu wa elimu kata wahakikishe wanasimamia mafundi ujenzi wa vyumba vya madarasa usiku na mchana ili wafunge taa za umeme.

Alisema katika wilaya hiyo, Rais Samia amepeleka fedha za miradi mbalimbali zaidi ya Sh. bilioni moja, hivyo lazima wamuunge mkono kwa kusimamia kazi za maendeleo.

Ofisa Elimu Msingi, Pili Maxmilian, na Ofisa Elimu wa Sekondari, Fredence Serapion na Mratibu Elimu Kata ya Genge, Peter Sanane, kwa nyakati tofauti walisema watahakikisha wanasimamia usiku na mchana miradi hiyo ambapo kwa sasa vyumba vya madarasa vimefikiwa hatua ya kupauliwa.

Miradi mingine iliyotembelewa ni pamoja na shule za msingi za kijiji cha Kwakifua, Mafere na Ngarani.

Pamoja na ukaguzi huo, kamati hiyo ilipanda miti ikiwa ni maadhimisho ya kumbukumbu ya mashujaa waliopigana vita na kuikomboa nchi.

# Kampeni msaada kisheria ya Mama Samia kila mwezi

**Na Ibrahim Joseph,** SONGEA

WAZIRI wa Katiba na Sheria, Dk. Damas Ndumbaro, amesema kampeni ya huduma ya msaada wa kisheria ya Mama Samia (Mama Samia Legal Aid Campaign) kuanzia sasa itafanyika nchi nzima kila Jumamosi ya mwisho wa mwezi ili kutatua kero za wananchi walizo nazo.

Akizungumza na waandishi wa habari mjini hapa juzi, Dk. Ndumbaro alisema hatua hiyo imelenga kuhakikisha kampeni hiyo inakuwa endelevu.

"Hatutaki tufanye kampeni hii kusiwe na uendelevu. Kila Jumamosi ya mwisho wa mwezi wakuu wa wilaya wa Tanzania Bara na Zanzibar watakuwa na jukumu la kuratibu kutoa elimu ya msaada wa kisheria kwa kuungana na asasi za kiraia.

"Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan ameshaleta suluhusho, atakayetuzingua na sisi tutamzingua, hatuwezi kukubali mtu ambaye ameajiriwa lakini hatekelezi wajibu wake vizuri muda wa kumsumbua mwananchi mtanzania mnyonge sasa umekwisha," alisema.

Waziri alisema kampeni hiyo itaendelea kuzinduliwa kila Mkoa huku utaratibu wa kila Jumamosi ukiendelea kufanyika.

Alisema kampeni hiyo iliyozunduliwa mwisho wa wiki iliyopita na Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, imeendelea kutoa fursa kwa timu ya wataalamu wa kisheria kufika maeneo mbalimbali ya mkoa huo kutatua kero za wananchi.

Kampeni hiyo, alisema ilikusudiwa kuwafikia wananchi zaidi ya 60,000 lakini matokeo yanaonyesha kuwa idadi itazidi kutokana na mwitikio mkubwa wanaojitokeza kupata huduma katika maeneo mbalimbali ya mkoa.

Alisema wananchi wengi wametatuliwa migogoro na kero walizo nazo kupitia wataalamu hao.

Waziri huyo alivishukuru vyombo vya habari kwa kuwa mstari wa mbele katika kuibua matatizo kwenye jamii hasa unyanyasaji wa kijinsia na mengineyo.



Ofisa Mtendaji Mkuu wa Tigo Pesa, Angelica Pesha akizungumza wakati wa uzinduzi wa huduma iliyoboreshwa ya mikopo kupitia simu za mkononi ya Nivushe Plus kwa kushirikiana na benki ya Azania, jijini Dar es Salaam juzi. Kulia ni Mkuu wa Kitengo cha Benki Kidijitali wa benki hiyo, Vinesh Davda. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wahitimu afya wafundwa matumizi mitandao

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

KATIBU Mkuu Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Adolf Ndunguru, amewataka wahitimu wa kada ya afya kujiepusha na matumizi mabaya ya mitandao ya kijamii ambayo ni kinyume cha maadili.

Aidha, amewakumbusha kutumia mitandao hiyo kwa ajili ya kupata maarifa na nyenzo mpya katika utendaji kazi wao sambamba na kuzingatia utoaji wa huduma bora.

Ndunguru aliyasema hayo jana mjini hapa katika mahafali ya 56 ya Chuo cha Afya na Sayansi Shirikishi Kibaha ambacho kiko chini ya Shirika la Elimu Kibaha (KEC).

Alisema, wahitimu wanatakiwa kuzingatia kuwa na matumizi mazuri ya mitandao ya kijamii kwa manufaa yao ambayo itawasaidia badala ya kuitumia kinyume na kuwaondoa kwenye maadili.

Katibu mkuu huyo pia aliwakumbusha wahitimu hao kuzingatia kuokoa maisha ya watu katika utendaji kazi wao badala ya kuangalia maslahi yao.

"Utabibu na uuguzi ni zaidi ya taaluma lakini pia ni wito. Itikieni wito kutoka kwa Mwenyezi Mungu na kuutumikia kwa weledi na uadilifu na mkifanya hivyo mtapata thawabu," alisema.

Ndunguru pia alitoa wito kujiepusha na lugha zisizofaa kwa wagonjwa na kejeli na mizaha wakiwa kazini huku akiwataka wajenge uadilifu na weledi kwa wagonjwa wanaowahudumia na kwa kufanya hivyo, watakiheshimisha chuo na kutukuza kuanzishwa kwa Shirika la Elimu Kibaha.

Aliahidi kuwa vikwazo vilivyoainishwa vitatafutiwa ufumbuzi kwa kutafuta fedha ikiwa ni pamoja na kufanya ukarabati.

Mkurugenzi wa Shirika la Elimu Kibaha, Robert Shilingi, alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kutoa Sh. bilioni 1.2 kwa miaka miwili ambazo alisema zimetumika kufanya ukarabati wa shule za Tumbi Shule ya Msingi, Mabweni ya Sekondari ya Wasichana Kibaha, Chuo cha Maendeleo na Shule ya Sekondari Tumbi.

Mkuu wa Chuo cha Afya na Sayansi Shirikishi Kibaha, Dk. Tusekile Solile, alisema upanuzi wa chuo hicho unahitajika ili kudahili wanachuo wengi zaidi.

Pia, alisema chuo kinakabiliwa na uhaba wa kompyuta na mabweni hali ambayo inasababisha baadhi ya wanafunzi kufuata malazi nje ya chuo.

Akisoma taarifa ya wahitimu, Irene Komba alisema chuo kinakabiliwa na ubovu wa vyoo, vyumba vya madarasa, viti na meza ambavyo vinahitaji ukarabati.

Risala ya wahitimu pia ilieleza kuwapo kwa uhaba wa nyenzo za kufundishia, hivyo wakapendekeza kuongezwa idadi ya vyumba vya kusomea, kuongezwa kozi na kuwapo kwa mfuko wa fedha.

# Waandishi habari waitwa kupatiwa mafunzo ya JKT

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MKUU wa Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), Meja Jenerali Rajabu Mabele, amesema wako tayari kupokea waandishi wa habari watakaohitaji kujiunga na mafunzo yanayotolewa katika kambi zao ili kuwajengea uzalendo.

Meja Jenerali Mabele, alisema hayo jana jijini hapa wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu utekelezaji wa majukumu ya JKT na mwelekeo wake katika mwaka wa fedha 2023/2024.

Alisema, Jeshi hilo lipo tayari kupokea waandishi wote nchini ambao watahitaji kujiunga mafunzo ambayo yanatolewa kwenye kambi mbalimbali nchini ili kuwapatia fursa ya kujifunza vitu mbalimbali ambavyo vitawajenga kuwa wazalendo wa nchi yao.

"Mimi nipo tayari kuwaandalia programu nzuri ya mafunzo wanahabari wote nchini ambao watakuwa tayari kujiunga na mafunzo yanayotolewa na jeshi hili katika kambi zetu mbalimbali mkiwa tayari tunawakaribisha sana," alisema Meja Jenerali Mabele Alisema katika mwaka huu wa fedha JKT, imetengewa Sh. bilioni 9.96 kwa ajili ya kujenga miundombinu na kuongeza kambi zingine kwa ajili ya kuongeza idadi ya vijana wanaopatiwa mafunzo kwa mujibu wa sheria, wa mkataba pamoja na mafunzo ya hiyari.

"Tunaishukuru sana serikali yetu kwa kututengea kiasi hicho cha Sh. bilioni 9.96 kwa ajili ya kuboresha miundombinu yetu ya makambi ili kusaidia kuongeza idadi ya vijana ambao wanapata mafunzo kila mwaka hasa hawa wa mujibu wa sheria wanaohitimu kidato cha sita kila mwaka," alisema. Alisema katika kipindi cha mwaka jana JKT, ilipokea vijana waliohitimu kidato cha sita 26,000 na mwaka huu imepokea vijana 52,119 ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 54.

"Mwaka 2022/23 serikali ilitupatia kiasi cha Sh. bilioni 7.5 kwa ajili ya uboreshaji wa miundombinu na kiasi hichi kilikuwa ni mara mbili ya kile kilichopita na hii inaonyesha azma ya serikali kuwezesha vijana wengi kupata mafunzo," alisema.

Pia, alisema katika kutekeleza azma ya Rais Samia Suluhu Hassan ya Tanzania kuwa kapu la chakula katika Bara la Afrika, wameweka mikakati mbalimbali ya kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula.

Katika mwaka huu wa fedha, Shilingi bilioni nne zimetengwa kwa ajili ya kujenga miundombinu ya umwagiliaji ili kuongeza maeneo ya kilimo na uzalishaji ili kukidhi hitaji la chakula kwa vijana na usalama wa chakula kwa taifa.

Kadhalika, alitoa wito kwa vijana nchini kuchangamkia fursa za mafunzo zinazotolewa na jeshi hilo ili kujipatia ujuzi wanaoweza kuutumia mara watakapo maliza mkataba wao wa miaka miwili ya kulitumikia Jeshi hilo.

"Hivi sasa tunazungumza na Wizara ya Kilimo kuona ni kwa jinsi gani ule mradi wa jenga kesho iliyo bora (BBT), kuunganishwa na vijana wanaohitimu mafunzo ya JKT ili kuwasaidia kupata shughuli za kufanya wanapomaliza mikataba yao ya miaka miwili na kukosa nafasi ya kuajiriwa na vyombo vya ulinzi na usalama nchini," alisema.

Mkurugenzi wa Idara ya Habari (Maelezo) na msemaji Mkuu wa Serikali, Gerson Msigwa, alilipongeza Jeshi hilo kwa namna linavyotoa mafunzo ya uzalendo kwa vijana na makundi mengine nchini.

"Meja Jenerali Mabele, niwapongeze kwa kazi nzuri mnayoifanya na mimi nitazungumza na vyama vya waandishi wa habari nchini kuona ni kwa namna gani tunaweza kuwapeleka JKT waandishi wetu waje wajifunze ili kuwa wazalendo watakapotoka huko hata karimu zao zitakuwa na uzalendo mwingi na taifa lao," alisema Msigwa.

# Wawekezaji walia gharama malighafi

**Na Friday Simbaya,** MAFINGA

BAADHI ya wawekezaji Mafinga mkoani Iringa, wameridhishwa na mazingira ya uwekezaji nchini, huku wakiiomba serikali kupunguza kodi za uagizaji malighafi kutoka nje ya nchi ili gharama ya uzalishaji ipungue.

Meneja Mkuu wa kampuni ya kuchakata mazao ya misitu ya YI SEN International Investment, Lin Xin Zong, alisema hivi karibuni kuwa mazingira ya uwekezaji nchini yameboreshwa tofauti na miaka ya nyuma.

"Ombi letu ni moja kwa serikali na mamlaka zinazohusika waangalie namna ya kupunguza gharama zilizowekwa kwenye uagizaji malighafi ambazo zinatumika kuzalishia bidhaa kwa mfano stika, kemikali, mbolea, ushuru wa forodha na gharama za usafirishaji ili bei zisifumuke sana," alisema.

Zong aliiomba serikali kuwaangalia kwa jicho la huruma wawekezaji wa mazao ya misitu ili kupunguza gharama za uzalishaji.

Kiwanda cha YI SEN kiko katika Kata ya Wambi eneo ya Luganga, mjini Mafinga na kilianzishwa mwaka 2020 lakini mwaka 2022 kilianza uzalishaji wa 'marine boards'.

Alisema kiwanda hicho kina ukubwa wa mita za mraba 4,000 za mradi pamoja na vitu vyote vilivyojengwa, yakiwamo maeneo ya vyumba vya makazi zaidi ya wafanyakazi 800.

Alisema kuwa soko lao la ndani la bidhaa za kampuni liko Tanzania na masoko makubwa ya nje ni pamoja na Kenya, Rwanda, Burundi, Malawi, Zambia na Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC).

"Kwa sasa ushindi ni mkubwa sana kwa sababu bidhaa kama ya marine boards imeanza kuzalishwa katika nchi jirani ndani ya Afrika Mashariki, lakini ili tuweze kushindana na masoko ya nje tunaomba serikali na mamlaka zinazo husika ziangalie namna ya kupunguza gharama za uagizaji malighafi zinazotumia kuzalishia bidhaa zetu,"alisema. "Tuna wafanyakazi wetu ambao wanatoka China pamoja na wazawa na tuna muundo wa uongozi wa wazawa 50 na uongozi wa wachina 10, lakini pia wafanyakazi wa ofisini wako 10 na maofisa masoko wa 05," alisema.

Kampuni ina wafanyakazi wa kudumu 500 na wafanyakazi wanaoingia na kutoka (casual workers) wako 300, hivyo kampuni imepunguza tatizo ya ajira kwa kiasi fulani.

Malighafi hizo ni pamoja na vigogo vya miti ya mikaratusi na vitu vingine vinatoka kwa wakulima wadogo na malighafi zingine zinatoka katika mashamba ya miti ya kupanda ya Sao Hill.



## HABARI DODOMA

# Viongozi wa dini waonywa kuhusu mafundisho ya chuki

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

MWENYEKITI wa Jumuiya ya Maridhiano na Amani Tanzania (JUMAT), Shekhe Dk. Alhad Mussa Salumu, amewakumbusha viongozi wa dini kujiepusha na mafundisho potofu yanayolenga kupandikiza chuki kati ya dini na dini, badala yake wahimize upendo, amani na mshikamano kwa Watanzania.

Aliyasema hayo juzi wakati akizungumza na viongozi wa jumuiya hiyo kutoka wilaya zote za Mkoa wa Dodoma ikiwa ni sehemu yake ya ziara ya kikazi ya kukutana na viongozi.

Akizungumza na viongozi hao alisema, hakuna dini yoyote inayofundisha chuki, kubaguana kati ya dini na dini bali zinaelekeza kuwapo kwa umoja, upendo na mshikamano kwa nia ya kujenga na kuwa kitu kimoja.

Alisema: "Nataka kuwaeleza wajumbe wa jumuiya hii kuwa kazi kubwa ni kuhakikisha tunalinda umoja wa nchi pamoja na kufundisha upendo ambao hauna viashiria vyovyote vya kubaguana wala kujengeana chuki kati ya dini na dini."

"Mitume wote walifundisha kuwa na upendo na amani kwa lengo la kila mmoja kumsaidia mwenzake pale anapokwama na kumuokoa katika shida alizonazo na mitume walikataza mtu kutumia mdomo wake kumsema vibaya mtu ambaye siyo wa dini yake wala kutumia mkono kumdhuru."

Akizungumza kuhusu mabadiliko ya katiba hiyo, alisema kwa sasa imeweka mambo tisa muhimu yatakayosimamiwa na jumuiya hiyo ambayo aliyataja kuwa ni pamoja na kupambania kulinda amani na utulivu kwa Watanzania, kutatua migogoro ya kidini na elimu juu ya kudumisha amani ya nchi iliyopo.

Alitaja mambo mengine ni pamoja na kusaidia juhudi za serikali katika suala la kimaendeleo, kuimarisha umoja wa nchi na wananchi, kutunza maendeleo ambayo yanafanywa pamoja na kusimamia mali ambazo hazihamishiki.

Naye Mwenyekiti wa Jumuiya hiyo Mkoa wa Dodoma, Askofu Dk. Evanci Chande, alisema viongozi wa mkoa huo watahakikisha wanasimamia misingi ya Katiba hiyo na wanatunza amani ya nchi, kujiepusha na migogoro ya kidini.

# Watoto 900 kunufaika na mradi wa elimu jumuishi, ufundishaji

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WATOTO 900 wenye matatizo ya macho nchini wanatarajia kunufaika na mradi wa elimu jumuishi na ufundishaji tembezi utakao tekelezwa na Shirika la Light for the World Tanzania, katika mikoa ya Dar es Saalam, Dodoma, Morogoro na Ruvuma kwa miaka mitano.

Mkurugenzi Mkazi wa Shirika hilo, Joseph Banza, alisema hayo juzi jijini hapa wakati wa ufunguzi wa kikao cha kwanza cha utekelezaji rasmi wa mradi wa elimu jumuishi na ufundishaji tembezi kwa watoto wenye matatizo ya macho katika mikoa ya Dodoma na Morogoro.

Banza, alisema katika utekelezaji wa mradi huo wametoa pikipiki 20 kwa ajili ya kuwawezesha walimu wa elimu maalumu ambao wanawasimamia watoto hao na vifaa mbalimbali vya kufundishia vya Sh. milioni 65.

"Shirika letu kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais TAMISEMI, wakuu wa mikoa ya Dodoma na Morogoro, Idara ya Elimu ya Msingi na Sekondari imeandaa kikao kazi cha watendaji wa elimu maalumu katika ngazi ya mikoa na halmashauri katika mikoa ya utekelezaji wa mradi wa elimu jumuishi kwa watoto wenye mahitaji maalumu hususani wenye changamoto ya uoni katika mikoa ya Dodoma na Morogoro," alisema.

Alisema lengo kuu ni kusisitiza uelewa, kupanga mipango na kutoa fursa ya majadiliano yanayohusu mradi wa elimu jumuishi na elimu maalumu kwa watoto wenye tatizo la uoni unatekelezwa katika halmashauri 14 ndani ya mikoa ya Dodoma na Morogoro kwa ufadhili wa Shirika la Light for the World.

Kadhalika, alisema malengo mahususi ya kikao hicho ni kutambulisha mradi mkubwa wa miaka mitano unaofadhiliwa na shirika hilo uitwao "Inclusive Vision 2022-2026," ambao unatekelezwa katika mikoa ya Dar es Salaam, Morogoro, Dodoma na Ruvuma.

Alisema malengo mengine ni kutoa maelezo ya kina juu ya elimu jumuishi na elimu maalumu kwa watoto wenye mahitaji maalumu na kutoa fursa kwa washiriki kuuliza maswali na kupata ufafanuzi kuhusu mradi huo. Vilevile, alisema mradi huo umekabidhi pikipiki 20 za kuwawezesha waalimu wa elimu maalumu ili waweze kutimiza majukumu yao kama waalimu tembezi kwa ubora na ufanisi.

"Jumla ya pikipiki 20 zimegawiwa katika mgawanyo wa mikoa ambapo pikipiki 12 zimetolewa kwa walimu kutoka mkoani Morogoro na nane kwa walimu wa Mkoa wa Dodoma na gharama ni Sh. milioni 49."

"Pia pikipiki hizo zina bima kubwa pamoja na vifaa mbalimbali vya kufundishia watoto wenye changamoto ya uoni hafifu na mahitaji maalumu vya Sh. milioni 16 na kufanya gharama yote kuwa Sh. milioni 65," alisema Banza. Kaimu Mkurugenzi Elimu Maalumu Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), George Mbijima, alisema tatizo la watoto wenye mahitaji maalumu nchini ni kubwa, hivyo wazazi wametakiwa kutowaficha ili wapate haki ya elimu.

Aliwataka watendaji kuwapatia elimu watoto wenye mahitaji maalumu kama mwongozo na sera ya elimu unavyotaka ili kupunguza tatizo hilo katika jamii.

Pia, aliwaomba waliopatiwa vifaa hivyo kuvitumia kwa malengo yaliyokusudiwa ili viwe na tija kwa taifa.



Waziri wa Viwanda na Biashara, Dk. Ashatu Kijaji (katikati), akikagua mbolea inayotengenezwa na Kiwanda cha Intracom mkoani Dodoma alipotembelea kuona shughuli za uzalishaji juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# CCM yaagiza waliokwamisha ujenzi kituo cha afya kuadhibiwa

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Singida, kimewagiza viongozi wa serikali wilaya ya Singida kuchukua hatua za kisheria dhidi ya watumishi waliosimamia ujenzi wa kituo cha afya cha Unyabwa, Manispaa ya Singida.

Serikali ilitoa Sh. milioni 500, lakini fedha zote zimeisha na mradi haujakamilika.

Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Singida, Martha Mlata, alitoa agizo hilo juzi baada ya wajumbe wa kamati ya siasa ya Mkoa wa Singida kukagua mradi huo na kubaini ujenzi kukwama kwa miaka miwili.

Baadhi ya wajumbe wa kamati hiyo walielezwa kuwa baada ya Sh. milioni 500 ambazo ili zitosheleze kumaliza mradi huo na huduma zianze kutolewa.

Walisema hivi sasa Manispaa ya Singida katika mwaka huu wa fedha imelazimika kutenga Sh. miliomi 90 ili zimalizie ujenzi wa kituo hicho.

Aidha, Mlata alihoji endapo Mkuu wa Wilaya ya Singida aliagiza Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) ilipewa kazi ya kuchunguza utata wa fedha hizo zilivyotumika.

"Rais Samia Suluhu Hassan alitoa fedha akitegemea mradi huu ukamilike kwa wakati hu wananchi waanze kupata huduma za afya sasa ni kwanini uchunguzi umechukua muda mrefu, naagiza kama TAKUKURU nao ni kikwazo kwenye mradi huu nao wachukuliwe hatua," alisema.

Naibu Meya wa Manispaa ya Singida, Hassan Mkata, alisema kutokana na utata wa matumizi ya fedha za ujenzi wa kituo hicho hatua za awali zilichukuliwa kwa kumwondoa Ofisa Mtendaji wa Kata aliyekuwa akisimamia ujenzi wa mradi huo.

Naye Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Singida Mjini, Lucia Mwiru, alisema Kamati ya Siasa ya wilaya hiyo ilipotembelea mradi huo ilikataa kuupokea kutokana na upungufu ikiwamo matumizi yasiyoeleweka ya Sh. milioni 500.

Mradi wa ujenzi wa Kituo cha Afya Unyabwa, ambacho kinatarajia kuhudumia zaidi ya wananchi 13,000 ulianza kutekelezwa Mei 2021 baada ya serikali kutoa Sh. milioni 500.





## ACT-Wazalendo yapinga uwekezaji Bandari Malindi

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

CHAMA cha ACT-Wazalendo kimesema haikuwa sahihi kwa serikali kubinafsisha Bandari ya Malindi kwa kampuni moja kutoka Ufaransa siku chache tangu Shirika la Bandari Zanzibar (ZPC) kununua vifaa vya kushusha na kupakia mzigo vya Sh. bilioni 13.

Hayo yameelezwa na Mjumbe wa Kamati Kuu ya chama hicho, Ismail Jussa, alipokuwa akihutubia mkutano wa hadhara uliofanyika Uwanja wa Chumbuni Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja.

Alisema vifaa hivyo vilinunuliwa kwa madhumuni ya kuimarisha huduma za Bandari na kama serikali ilikuwa na mpango wa kubinafsisha wasingenunua vifaa hivyo.

Jussa alisema mwekezaji ndiye alipaswa kununua vifaa vyake kama kweli ameamua kuwekeza kwa madhumuni ya kuimarisha huduma za Bandari ya Malindi Zanzibar.

Aidha, alisema mbali ya fedha hizo shirika kabla ya kubinafsishwa lilitumia dola za Marekani milioni sita kuweka mfumo wa huduma za mtandao kiwango ambacho ni kikubwa hasa kwa kuzingatia udogo wa Bandari ya Malindi Zanzibar

'Dola milioni sita kwa Bandari ya Malindi lakini mfumo kama huo umewekwa Bandari ya Dar es salaam kwa gharama ya dola za Marekani 460,000.

Aidha, alisema kuna kampuni tatu zimepatiwa kazi ya kutoa makontena bandarini na kupeleka katika eneo la bandari ya nchikavu katika eneo la Maruhubi na kila kontena moja linatozwa Sh. 150,000 kutoka Malindi hadi Maruhubi wakati umbali haufiki kilomita moja.

Jussa alisema wafanyakazi katika Bandari ya Malindi wanafanyakazi katika mazingira magumu baada ya kutakiwa wafanyekazi kwa muda wa saa nane baada ya hapo wanatakiwa kufanya kazi kwa malipo ya muda wa ziada kwa Sh. 8,000 kwa siku.

Akizungumzia mradi wa maduka wa Darajani, Jussa alisema gharama wanazotozwa wafanyabiashara katika tozo ya pango haifanani na gharama za mradi na badala yake kuwanufaisha wawekezaji wa mradi huo.

Jussa alisema wawekezaji wa mradi huo wametumia gharama za ujenzi Sh. bilioni 6.2 na huku wakitakiwa kujilipa kwa muda wa miaka 33 kwa mujibu wa mkataba wa uwekezaji wa mradi huo.

Makamu Mwenyekiti wa chama hicho, Othman Masoud, alisema chama chake kimejenga utamaduni kuendelea na wajibu wa kuichunga serikali.

Othman ambaye ni Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar alisema 'Zanzibar haiwezi kupiga hatua ya maendeleo bila ya kuwa na mamlaka kamili yatakayotoa fursa ya kujiamulia mambo yake ya kiuchumi."

# Mfumo wa ikolojia kusaidia ukusanyaji mapato utalii

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MFUMO wa ikolojia wa kidijitali kwa sekta ya utalii Zanzibar umetajwa utasaidia usalama wa ukusanyaji wa mapato yatokanayo na sekta ya utalii.

Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya Vantagepay kutoka Londan, Barry Lobel, aliyasema hayo visiwani Zanzibar wakati wa mkutano wa kuutambulisha mfumo huo.

Alisema anatambua kwamba Serikali ya Zanzibar imeanzisha mifumo mbalimbali ya kidijitali ili kuimarisha uwajibikaji, akisema teknolojia yao haitabadilisha chochote katika usimamizi na uendeshaji wa mifumo iliyopo.

Lobel alisema teknolojia wanayotumia ina kiwango cha kimataifa, ambayo itaifanya Zanzibar kuwa miongoni mwa mataifa yatakayonufaika na huduma zao.

Alisema akiwa Zanzibar amepata fursa ya kujadiliana na wataalamu juu ya mifumo inayotumika na kuangalia uwezekano wa kushirikiana kuiimarisha.

Mwakilishi wa Taasisi ya Initianova kutoka jijini Dar es Salam, Ansel Misango ambao wasimamizi wa mfumo huo, alisema kuzinduliwa kwa mfumo huo utaisaidia serikali na sekta binafsi katika ukusanyaji wa kodi hasa kwa sekta ya utalii.

Alisema lengo la kufika Zanzibar kuanzisha mfumo huo ni kutokana na sera nzuri za Rais Dk. Mwinyi kwa kutoa fursa nzuri kwa wawekezaji kwenye sekta ya kidijitali.

Alisema fursa hiyo ni nzuri na imewavutia kuwekeza Zanzibar katika teknolojia hiyo ambayo pia itasaidia kupatikana kwa taarifa za wageni wanaofika Zanzibar.

"Mfumo huu utasaidia watalii wanapoingia na wanapotoka Zanzibar wanakaa kwa muda gani lakini kujua usalama wao,"alisema.

Katibu Mtendaji wa Baraza la Udhibiti wa Mfumo wa Utoaji Leseni kutoka Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda Zanzibar, Hawa Ibrahim, alisema kuanzishwa kwa mifumo ya ulipaji huduma na ukusanyaji wa kikodi kwa njia ya kidijitali itachangia kasi ya ukusanyaji wa kodi.

Alisema lengo la Serikali ya Zanzibar ni kuendana na mfumo wa kidijitali, hivyo ni vyema kuwa na mifumo ya kikodi, kibiashara na kimasokko ambayo itaendana na hali halisi ya uchumi wa kimataifa.

Aidha, alisema lazima kuwapo na mfumo ambao utasaidia mfumo wa awali kutambulika katika usajili wa wageni na wazawa waliopo nchini.

Alisema ujio wa Kampuni ya Initianova utaipelekea Zanzibar sehemu nzuri yenye mafanikio na kuwa na uchumi endelevu.

Alisema Zanzibar imefunguka zaidi katika uwekezaji na eneo ambalo linahitaji kuwekezwa zaidi ili kupata manufaa zaidi ni sekta ya utalii ambayo ndio sekta mama na huduma ya mifumo ya kidijitali ambapo uwekezaji bado haujafikia katika kiwango kizuri cha kigigitali.



Mwakilishi wa Jimbo la Bububu, Mudrik Ramadhan Soraga (wa pili kulia), akiwasalimia wananchi wa jimbo hilo Zanzibar juzi, alipofanya ziara ya kusikiliza changamoto zao na kuzitatua. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# 'Walimu wana wajibu wa kufundisha afya ya uzazi'

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MRATIBU wa mradi wa kutengeneza mazingira rafiki kwa wasichana shuleni, Ester Mwakalobo, amesema licha ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kuwapatia haki ya elimu watoto wa kike lakini walimu wanawajibu wa kuwafundisha wanafunzi masuala ya afya ya uzazi.

Aliyasema hayo wakati akifunga mafunzo ya siku tatu kwa walimu wa Shule ya Sekondari ya Fukuchani Mkoa wa Kaskazini Unguja.

Alisema katika kuhakikisha mtoto wa kike anashinda ndoto zake za kufanikiwa kielimu ni lazima kujengewa msingi mzuri juu ya afya ya uzazi kwa sababu wanafunzi wa kike wanachangamoto katika eneo hilo.

Alisema baada ya kuona uelewa mdogo wa wasichana kuhusu afya ya uzazi wameamua kuwa na mradi huo unaofadhiliwa na Shirika la Ushirikiano wa Kimataifa la Korea (KOICA) na Taasisi ya Korea Food for the Hungry International (KFHI) ili kuwapa walimu mafunzo hayo na kuwafundisha wanafunzi shuleni. Alisema wameamua kuwapa mafunzo walimu kwa sababu ni walezi na muda mwingi wanakuwa na wasichana shuleni, hivyo anaimani kuwa malengo yatafikiwa katika kufikisha elimu ya afya ya uzazi.

Alisema mradi huo unafanya kazi katika shule tano kwa Zanzibar ikiwamo shule tatu kutoka Unguja na shule mbili Pemba ambazo ni Fukuchani, Jendele na Mtule, Shumba Viamboni na Kichaka Tumbe.

Alisema elimu hiyo itawasaidia wasichana kujitambua na kuepukana na mimba na ndoa za utotoni ambazo hukatisha ndoto zao ikiwamo za kielimu.

Akitoa mafunzo kwa walimu hao Mkurugenzi wa Jinsia wa KFHI, Rosemary Mfui alisema walimu wanawajibu wa kukemea masuala ya mahusiano kwa wanafunzi ili kuondokana na changamoto ya afya ya uzazi wakati wapo katika umri mdogo.

Alisema walimu wananafasi kubwa ya kuwafundisha wanafunzi wa kike juu ya ustadi wa maisha yao na wanafunzi wengi hawana elimu ya stadi ya maisha.

Alisema wasichana huathirika kisaikolojia baada ya kufanyiwa vitendo vya udhalilishaji ikiwemo kupewa ujauzito, hivyo walimu wanatakiwa kuwatambua wanafunzi hao na kuwapa ushauri nasaha na sio kuwakaripia. Walimu waliopatiwa mafunzo hayo walisema mradi huo unaumuhimu mkubwa kwa walimu na wanafunzi wa kike katika makuzi yao hasa katika kupata elimu ya kujitambua na kuondokana na changamoto za afya ya uzazi.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Fukuchani, Mwamini Khamis Juma alisema umri wa balehe ni hatari kwa mtoto wa kike na kiume, kwamba ni muda ambao hupambana na vishawishi vinavyosababisha kudhalilishwa.



KAJALA

UKURASA 12

Nipashe
MWANGA WA JAMII

BT
BURUDANI TELE

JUMAMOSI JULAI 29, 2023



# IWE JUA IWE MVUA

UKIIONA kapo mpya ya mastaa, Marioo na Paula unaweza kusema wamependezana, kinachohitajika ni kuhalalisha tu kwa kufunga ndoa takatifu.

Marioo ambaye ni mwanamuziki pendwa nchini na Paula ambaye ni binti wa mwigizaji maarufu, Kajala Masanja wameteka kwa muda mitandao ya kijamii kutokana na kuongoza kwa kujadiliwa kupita mastaa wengine.

Hata hivyo, mashabiki wa mastaa hao wamegawanyika katika kulijadili penzi hilo, kuna wale wanaowatakia kila la heri katika safari yao, huku wengine wakiwa na mashaka na uhai wake.

Mwanamuziki huyo tangu alitangaze penzi lake hadharani, ameonekana kuwa na hari ya kufanya kazi, kiasi ambacho amewashangaza watu baada ya kutoa ngoma kali mfululizo.

Watu wanaomuunga mkono wanasema Paula ameweza kumuongezea nguvu kutokana na mahaba mazito anayompatia na kumfanya kijana huyo kutoka Rufiji, anapata nguvu ya kufikiria kazi pekee na sio mambo mengine.

Hivi karibuni Marioo ametoa ngoma kwa jina la 'Love Song' na kuipakia kwenye YouTube yake.

Baadhi ya watu ambao wana mashaka na penzi lao, wamebainisha kwamba mastaa wengi walioanzisha uhusiano waliishia kuangukia pua, kutokana na mmoja wao kuwa na tamaa ya kutaka kupata zaidi.

Walitolea mfano wa uhusiano wa Kajala Masanja na Harmonize, ulikufa ghafla mara mbili na kisha kila mmoja kutoa sababu zinazoashiria walipokuwa wakiishi walikuwa na matumaini tofauti zaidi ya kuimarisha mapenzi yao.

Hata hivyo, mwenyewe alikaririwa akisema kuwa wanaozungumzia tofauti kuhusu uhusiano wake na Paula, hawataweza kuwatenganisha na kuapa kwamba iwe mvua au jua, watazidi kuchanua na kuimarika.

Ikumbukwe Kajala amekuwa akisema Marioo ni mkwe wake baada ya msanii huyo kuweka wazi yeye na Paula ni mtu na mpenzi wake.

BASI SAWA

## Nay Wa Mitego kibano tena

RAPA ambaye hakosi hekaheka kila anapotoa ngoma, Nay wa Mitego, amejikuta akilalamika kuonewa baada



ya Baraza la Sanaa Tanzania, kumwita kwa ajili ya mashauriano.

Akizungumza na Ayo Tv, Nay wa Mitego, amesema barua ya wito ameipata, lakini kwa bahati mbaya yeye yuko safarini , hivyo mwanasheria amewasiliana kushughulikia tatizo hilo na kama itatolewa ratiba mpya atahudhuria.

"Sema tu kwa sababu watu hawapendi ukweli, ni wimbo ambao nimezungumza maisha ya kila mtu, hukumbuki utaratibu wa kupeleka wimbo usikilizwe kwanza ushatolewa, ilikuwa sio lazima, tutaangalia siku hiyo itakavyokua, mimi nafanya kwaajili ya jamii yangu" Amesema Nay wa Mitego

## Phantom Musica International waja na Tedy

KUNDI la muziki wa dansi la Phantom Musica wameipua kibao kipya kitakachojulikana kwa jina la Tedy.

Mkurugenzi Mtendaji wa kundi hilo linalofanya kazi kwa utaratibu wa 'Zing Zong', Abdulfareed Hussein amesema, wimbo huo umerekodiwa chini ya Prodyuza Erasto Mashine wa jijini Dar es Salaam.

Wimbo huu ambao ni utunzi wa Edo Sanga unakamilisha idadi ya nyimbo tisa ambazo tayari wamesharekodi hadi sasa.

Amesema, Kukamilika kwa wimbo Tedy ni mkakati wa Phantom Musica International kukamilisha albamu itakayokuwa na jumla ya nyimbo kumi na mbili.

"Matarajio ni kukamilisha albamu na Tedy ni sehemu ya nyimbo zitakazokuwa ndani ya dhamira yetu hii.





## KUMBE KAJALA KALA CHUMVI

MWIGIZAJI maarufu wa Bongo Muvi, Kajala Masanja, amesema pamoja na kuonekana ana umbo kama binti mdogo, ana miaka 40 ambayo inamfanya kuwa mtu mzima kwa sasa.

Amesema hana sababu ya kuficha umri wake kama wanavyofanya wasanii wengine kwa sababu anataka kuona kila mtu anayemfuatilia afahamu.

"Sioni sababu ya kuficha umri wangu, ni jambo la ajabu kukataa miaka yako na yule ambaye atakubali sawa na asiyetaka siwezi kumlazimisha wala kumjibu kile anachokiamini," amesema Kajala.



## Diamond, Ali Kiba waliamsha

BIFU kati ya wanamuziki wakongwe nchini, Diamond na Alikiba unazidi kukita mizizi baada wiki hii wawili hao kujikuta wakijibizana mitandaoni.

Kupitia Instastori yake, Diamond ameamua kujibu mapigo kwa kueleza kuwa anapotoa ngoma yoyote, anatakiwa kufunga mdomo wake kwa sababu yeye hakurupuki kwani anafanya kazi kwa mkakati.

"Unapoona nimetoa ngoma yoyote, funga mdomo, maana sikurupuki, naachia ngoma kwa mkakati maalum," Diamond alifoka.

Wiki jana, Alikiba alimkosoa vikali Diamond kwa jinsi alivyofanya wimbo wake alioshirikishwa na Jux, "Enjoy" akisema kwamba msanii huyo anaudhalilisha muziki wa Bongo Fleva kwa kile alichodaiwa wizi wa kazi za sanaa za wasanii wa Nigeria.

## POVU LA ALIYEACHWA, BORA KUINJOI

**Na Adam Fungamwango**

"NIMEACHWA sitaki tena maswali, naenda bichi kula upepo wa bahari, naumwagilia moyo muziki kwa mbali, jimbo liko wazi sema nitakubali." Haya ni maneno kutoka kwenye wimbo wa Rayvanny aliyomshirikisha Diamond Platnumz, unaitwa 'Nitongoze.' Ni maneno ya mtu aliyeachwa na mpenzi wake.

Jux, akimshirikisha pia Diamond naye kwenye wimbo wake 'Enjoy' amerudia mle mle, hataki tena mapenzi, anachotaka ni kujipongeza tu, bora ainjoi kwa sababu maisha ni mafupi. Haya pia ni maneno ya mtu mwenye 'stresi' za mapenzi.

Kwa hali ya kawaida ya binadamu, kuachwa na mpenzi ni jambo baya sana ambalo hataki limtokee.

Unaweza kuomba ardhi ipasuke ili uingie. Mtu anayeachwa anaweza kuona kama dunia yote inamuonea. Ataomboleza na kuongea yote. Wanamuziki na wasanii wanalijua hili. Achana na Rayvanny na Jux, hata zamani wanamuziki walilia kuachwa.

**Kuachwa-Khalid Chokoraa**

Wimbo huu ulitoka katikati ya miaka ya 2000, utunzi wake Khalid Chokoraa. Unazungumzia jinsi mtu aliyeachwa anavyojisikia vibaya. Mbaya zaidi ni kumuona mpenzi wake aliyeamuacha ananenepa, halafu yeye anakonda kwa mawazo. Ni moja kati ya vitu vibaya na usiombe yakukute.

**Mama Rhoda-Jose Chameleone**

Mwanzoni mwa miaka ya 2000, msanii kutoka Uganda, Jose Chameleone, alitoka na wimbo unaosema 'Mama Rhoda'.

Mtunzi anamlalamikia mama Rhoda kwa nini amemuacha na anamwambia kuwa ipo siku atamkumbuka. Ni kwamba mama Rhoda amemkimbia na kumuacha na watoto.

**Shahada ya uvumilivu-DDC Mlimani Park**

Ni wimbo wa masikitiko sana. Ulitungwa katikati ya mwishoni mwa miaka ya 1980. Ni stori ya mtu anayetunukiwa shahada ya uvumilivu na rafiki zake. Ni baada ya kukimbiwa na mkewe ambaye alirubuniwa na mwanaume kwa ahadi ya pesa na kujengewa nyumba. Jamaa ilimuuma sana, lakini hakulipiza kisasi cha hasidi aliyemrubuni mkewe. Badala yake aliacha kama ilivyo, lakini akiugulia maumivu moyoni.

**Tuma-Juwata Jazz Band**



Katikati ya miaka ya 1980, Tx Moshi William alitunga wimbo wa 'Tuma', unaomzungumzia mtu aliyesimama kwenye kona ya barabara za Uhuru na Msimbazi akiatazama wanaokwenda na kurudi kama anaweza kumuona mpenzi wake Tuma walioahidiana kupelekana kwa wazazi.

Jua liliwaka, hadi lilizama, demu hakuonekana. Jamaa alikuwa amechwa kwenye mataa.

Kwa huzuni, jamaa anaona kuwa ni matatizo kumpenda mwanamke mrembo anayependwa na wengi, unaweza kunywa sumu au kujinyonga. Hata hivyo kwa kuwa yeye ni kijana, basi atasonga mbele na maisha mengine.

**Mchumba Hanitaki-Simba Wanyika**

Ilikuwa ni mwishoni mwa miaka ya 1970, Willson Peter alipotunga wimbo wa 'Mchumba Hanitaki.'

Jamaa analalamika kuwa mchumba wake awali alikuwa anampenda na walipanga kuoana, lakini kwa sababu sasa pesa na kazi hana, ameamua kumsaliti na kumkataa mchana kweupe.

Jamaa analalamika alie na nani.

FILAMU

# Chizi: Usilolijua Litakusumbua

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI mwingine kwenye dunia hii siyo kila unachokiona basi ndivyo kilivyo, hivyo lazima uwe makini sana.

Sitaki kuendelea kiundani sana ila tuingalie filamu hii iitwayo 'Chizi', ambayo inakupa mafunzo mbalimbali na kupata kufahamu mapya juu ya sayari hii ya dunia.

Mtu mmoja anakimbizwa na watu, akakutana na msichana mmoja akamtupia mkoba wake mdogo na kumwambia aufiche. Akafanya hivyo. Hata hivyo inamletea matatizo. Anaanza kuwindwa na watu wasiojulikana. Mara mbili anavamiwa na watu ambao hawajui, lakini kwa maajabu anasaidiwa na mtu mmoja ambaye anaonekana ana matatizo ya akili kutokana na mavazi yake na muonekano.

Baada ya kusaidiwa mara mbili chizi aliwatwanga wote waliokuwa wamemvamia, binti yake anaamua kumfuata hadi kwenye pagala analoishi. Chizi yule ambaye haongei anajaribu kumpa ishara kuwa aondoke pale, lakini msichana anakataa akisema yeye mwenyewe hana pa kwenda na kwa sababu amekuwa msaada mkubwa wake, hivyo ameamua kukaa pale.

Baada ya wiki moja, Chizi akaanza kuongea. Msichana akashtuka na kufurahi. Aliyeonekana kama Chizi akajitambulisha kwa jina la Samir na akasema ameamua kujiweka hivyo kutokana na kumuua mkewe kwa bahati mbaya baada ya kumfumania.

Akafanya hivyo ili kuepuka mkono wa sheria ambapo matendo yote aliyokuwa akiyafanya, kila mmoja akaamini kama ni chizi, hivyo ameamua kuishi maisha hayo kwani siku akijifanya mzima tu, atapelekwa kortini na kunyongwa.

Msichana naye akajitambulisha kwa jina la Eunice. Akajitambulisha kuwa yeye ni mtoto yatima aliyefiwa na wazazi wake wote na anaishi maisha ya kuokota makopo ili akauze ajipatie riziki. Kwa maana hiyo hana makazi maalum.


Samir akamuuliza kisa cha kuvamia mara kwa mara na vijana wake, akamueleza jinsi alivyopewa mkoba na mtu ambaye hamfahamu na huwa anauhifadhi kwenye kiroba anachowekea makopo anayookota. Kwa sababu waliamua kuishi wote hapo, mkoba ule akapewa Samir awe nao.

Mtu yule alikutana tena na Eunice njiani na kumpeleka kwa Samir. Akamwambia kwenye mkoba kuna flashi ambayo wenzake walitaka kuisambaza ili kumchafua msichana mmoja ambaye walimbaka. Akasema yeye aliamua kuiiba kwa kumtetea, ndiyo maana wenzake walikuwa wanamkimbiza.

Mtu yule aliyejitaja kwa jina la James aliichukua flashi hiyo kutoka kwa Samir na kumtafuta msichana mhusika ili amsaidie kwenye ushahidi polisi.

James akamtaka Samir aondokane na hali ile ya uchizi lakini mwenyewe alikataa katakata kwa madai ndiyo inayomfanya aishi uraiani, badala yake akataka amchukue Eunice ili asiishi maisha mabaya ya pale.





# Baba yake Drake atoa kali

BABA wa mwanamuziki maarufu wa Marekani, Drake, amewashauri watu wanaotaka kuanzisha familia wasiache kufanya mapenzi kwa kuwa hiyo ndiyo njia sahihi ya kuanzisha familia.

Akijibu swali kutoka kwa shabiki mmoja, Mzee Dennis Graham, alitoa ushauri huo baada ya shabiki huyo aliyeitwa Daniels kumuuliza kama yeye anaweza kupata mtoto siku moja.

Endelea kufanya mapenzi, Mzee Graham alijibu kwa ufupi kabla ya kutoweka ndani ya hoteli anayoimiliki katika jiji la New York City.



## Davido alijua kitakachotokea

WATU mbalimbali wametoa maoni kuhusu wimbo mpya wa Davido, unaoitwa Logos Olori, wengi wakisema mwanamuziki huyo alijua nini kitatokea.

Hivi karibuni meneja wake, Israel Afeare, maarufu kama Israel DMW, ameomba radhi jamii ya Waislamu kutokana na video hiyo yenye utata iliyopostiwa na bosi wake.

Kumbuka kwamba Davido alikumbwa na mzozo baada ya kuweka video ya wimbo huo, ikiwaonyesha watu waliokuwa wakiswali kwa njia ya Kiislamu na kisha kucheza wimbo huo msikitini.

Hata hivyo watu wengi wanaamini kwamba kabla hajaweka video hiiyo, Davido alijua nini kitatokea na hivyo ana wajibu wa kukabilaina nayo.

## Tupac bado anapendwa

Bado mapenzi kwa rapa maarufu marehemu Tupac Shakur, bado yametanda mioyoni mwa watu, baada ya pete yake iliyotengenezwa kwa dhahabu, rubi na almasi, kununuliwa kwa zaidi ya shilingi bilioni mbili.

Mnada huo ulifanyika huko New York siku ya Jumanne, ulishuhudiwa pete hiyo ikinunuliwa kwa bei ya kuvunja rekodi.

Rapa huyo mzaliwa wa New York alivaa pete hiyo mara ya mwisho kwenye Tuzo za Muziki za Video za MTV, Septemba 4, 1996.





## Flavour aona ni sawa

MWANAMUZIKI maarufu wa Nigeria, Chinedu Okoli, maarufu kwa jina la Flavour amemtoa hofu mwanadada mmoja aliyesema anataka kumpenda mwanaume wa Igbo lakini ana wasiwasi kuhusu mitindo yao ya mavazi.

Mwanamke huyo alielezea hofu yake kutokana na video ya mwimbaji huyo aliyevalia shati jeusi isiyo na mikono na suruali ya kamba, ambayo alichapisha kwenye ukurasa wake wa Twitter.

Msanii huyo baada ya kuona maoni yake akajibu, akisema, "Utakuwa sawa.".

## Bow Wow ukiruka hapo wewe kidume

MWANAMUZIKI wa Marekani, Bow Wow anakabiliwa na tuhuma ya kutapeli kiasi cha dola 3,000, sawa na shilingi milioni 7.4 kwa baba wa kijana aliyetaka kushirikishwa katika wimbo.

Katika kesi yake, Steven Roberson anadai alimpatia pesa hizo Bow Wow, mzaliwa wa Shad Moss, kupitia Cash App mnamo 2021, kama sehemu ya makubaliano yao ili kutoa kifungu cha wimbo "Daddy's Girl" aimbe mtoto wake.

Bow Wow alijibu mashtaka hayo akisema kuwa hajawahi kutumia Cash App na anajizuia kufanya biashara kupitia programu hizo.



## Upinzani watakiwa kushirikiana uhamasishaji Dira Taifa Maendeleo

**Na Hamida Kamchalla,** TANGA

VIONGOZI wa vyama vya upinzani vya siasa wametakiwa kutoa ushirikiano wa dhati na kushiriki kikamilifu kwenye uhamasishaji wa maandalizi ya Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2050.

Akifungua mkutano wa uhamasishaji wa ushiriki wa wadau katika maandalizi ya dira hiyo, Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Waziri Kindamba, alisema viongozi wa vyama pinzani wanahitajika kutoa mchango wao ili inapotengenezwa dira hiyo isaidie wao kutembea nayo ikitokea wameingia madarakani.

"Viongozi wa vyama pinzani tunahitaji mchango wenu ili tunapoitengeneza dira hii hapo baadaye ikitokea kama mtashika madaraka mtembee nayo katika uongozi wenu, iwe ni dira ambayo imejumuisha makundi yote.

"Tanzania ni yetu sote, kila mmoja anapaswa kutoa mchango wake inavyostahiki, wasitokee wengine wakajiona kuwa wana haki zaidi kuliko wengine kwa kuwa wote ni wajenzi wa nyumba moja hakuna haja ya kugombania fito," alisema.

Aidha, alisema Dira ya Taifa ya Maendeleo, inagusa makundi yote na anatarajia kutakuwapo kwa ushirikishwaji kwa wadau wote katika ngazi zote ikiwamo taasisi za elimu ya juu ya utafiti, sekta binafsi, asasi za kiraia na wananchi mmoja mmoja.

Alisema kuwa dira hiyo itakuwa na umuhimu mkubwa kwa kuwa itasaidia kutoa taswira halisi ya nchi kuelekea miaka ijayo, pia itakuwa sehemu ya kuonyesha mipango halisi ya kimaendeleo kwa nchi na wananchi.



Wakazi wa Wilaya ya Muheza mkoani Tanga wakipanga foleni ya kununua mafuta katika kituo cha Mnyamuru mkoani Tanga wiki hii, baada ya bidhaa hiyo kuwa adimu. Bei ya lita moja ya petroli iliuzwa kwa 4,000/-. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

## UNDP kushirikiana na wanahabari miradi athari mabadiliko tabia nchi

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

SHIRIKA la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP), kupitia programu ya miradi midogo (SGP) nchini, limeahidi kuendelea kushirikiana na Taasisi ya Wanahabari ya Kusaidia Jamii za Pembezoni (MAIPAC), kutekeleza miradi ya kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi, utunzaji wa mazingira, misitu na vyanzo vya maji.

Maofisa wa UNDP, kupitia programu ya SGP, pamoja na maafisa wa Taasisi ya Jumuiko la Maliasili Tanzania TNRF, wametembelea ofisi ya MAIPAC jijini Arusha, kufanya tathmini ya utekelezaji wa mradi wa uhifadhi wa misitu, maji na mazingira kwa maarifa ya asili, uliokuwa unatekelezwa na MAIPAC katika Wilaya za Longido, Monduli na Ngorongoro, mkoani Arusha.

Juzi, akizungumzia utendaji wa MAIPAC, Ofisa Programu wa SGP wa UNDP Tanzania, Faustine Ninga, alisema wameridhishwa na MAIPAC jinsi ilivyotekeleza mradi huo, ambao ulikuwa unadhaminiwa na Mfuko wa Mazingira Duniani (GEF) na wadau wengine wa maendeleo.

"Hapa sisi tumekuja kuona jinsi mlivyotekeleza mradi wenu, kwa ujumla tunawapongeza sana kwa kuwa mmefanya kazi nzuri kuzifikia jamii za pembezoni na kukusanya maarifa mengi ya asili na baadaye kutoa katika vyombo vya habari na kuandaa vitabu," alisema.

Aidha, alisema taasisi hiyo imefanikiwa kufikisha ujumbe maeneo mbalimbali kuhusu umuhimu wa maarifa ya asili kwa uhifadhi wa mazingira, vyanzo vya maji na misitu pia kushirikiana na taasisi nyingine ikiwamo za serikali kutoa elimu ya uhifadhi wa mazingira.

"Tunaahidi tutaendelea kufanya kazi pamoja, kikubwa muendeleze kutoa elimu kwa maarifa ambayo mmekusanya, pia kubainisha fursa nyingine ambazo mnaona tunaweza kushirikiana ili kusaidia jamii," alisema.

Kaimu Mkurugenzi wa TNRF, Steve Ngowi, Mratibu wa miradi alisema taasisi hiyo imefanyakazi nzuri ikiwamo kushirikiana kutoa habari na machapisho ya mashirika mengine, ambayo yalikuwa katika progamu ya miradi inayosaidiwa na UNDP.

Naye Mkurugenzi wa MAIPAC, Mussa Juma, alishukuru UNDP kupitia programu ya SGP na TNRF kushirikiana na MAIPAC kutekeleza mradi wa uhifadhi wa mazingira, vyanzo vya maji na misitu kwa maarifa ya asili.

Hata hivyo, alisema mradi huo, umetekelezwa kwa mwaka mmoja kwa manufaa makubwa na jamii imeshirikishwa ikiwamo Halmashauri za Wilaya ya Longido, Monduli na Ngorongoro, pia serikali kuu hasa Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira, Dk. Selemani Jafo, ambaye alizindua vitabu ambavyo walichapa kuhusu maarifa ya asili.

Meneja Miradi na Utawala wa MAIPAC, Andrea Ngobole, alisema wana imani wataendelea kushirikiana zaidi na mashirika na taasisi nyingine, Serikali ya Ujerumani na wadau wengine katika kutekeleza miradi ya kusaidia jamii, zikiwapo za pembezoni.

Watendaji wa UNDP na kushirikiana TNR, wako katika ziara ya kukagua na kufanya tathimini ya utekelezaji wa miradi midogo kwa mashirika 13 ambayo yalipatiwa fedha na UNDP kutekeleza miradi hiyo nchini.

## CCM yaridhishwa utekelezaji miradi maendeleo

**Na Allan Isack,** ARUMERU

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM), Wilaya ya Arumeru mkoani Arusha, kimeridhishwa na utekelezaji wa ilani ya chama hicho,kwa ujenzi wa miradi ya maendeleo katika Halmashauri ya Arusha wilayani humo.

Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Arumeru, Noel Severe, alisema hayo kwenye halmashauri hiyo, wakati wa uzinduzi wa jengo la maabara ya masomo ya sayansi katika Shule ya Sekondari Oldonyowas.

Ujenzi wa mradi wa maabara hiyo, uliotekelezwa kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), kwenye shule hiyo ya sekondari.

Alisema serikali imetoa fedha nyingi za utekelezaji wa miradi ya maendeleo kisekta katika halmashauri hiyo.

Pia ina matarajio makubwa itakayokwenda kuleta matokeo chanya kwa wananchi.

Alisema ameridhishwa na ujenzi wa miradi hiyo kwa kuwa utekelezaji wake umezingatia viwango vya ubora unaoendana na thamani halisi ya fedha zinazotolewa na serikali kwa kuwa ni utekelezaji wa ilani ya CCM ya mwaka 2020/2025.

"Ninawapongeza kwa kazi nzuri mnazozifanya, pia wataalamu kwa usimamizi wa miradi ya maendeleo, imezingatia viwango na ubora kulingana na thamani ya fedha 'Value for Money' na imeleta matokeo chanya ya utoaji na upatikanaji wa huduma kwa wananchi.

Aliwapongeza wananchi kwa ushiriki wao utekelezaji wa miradi hiyo, kwa kujitolea nguvu kazi kwenye shughuli za ujenzi pamoja na usimamizi wa miradi iliyojengwa kwa kuwatumia Mafundi Jamii 'Force Account'.

Alitoa rai kwa wanafunzi kusoma kwa bidii kwa kuwa serikali itahakikisha kila mwanafunzi anapata elimu ya msingi kuanzia darasa la awali mpaka kidato cha nne bila malipo karibu na makazi yao kwa kuwa tayari serikali imeshatekeleza jukumu hilo.

Vilevile, alisema awali jamii za kimaasai watoto wa kike hawakupata fursa ya kupata elimu ya sekondari, kutokana na mila na desturi na uchache wa shule kwa nyakati hizo, lakini kwa sasa serikali imejenga shule za sekondari kila kata na kutoa fursa kwa kila mtoto kupata nafasi ya kujiunga na masomo ya sekondari.

"Niwatie moyo wasichana, someni kwa bidii, wanawake mnaweza, hakikisheni mnatumia fursa hii adhimu ili kufikia ndoto zenu, tunatarajia kupata wataalamu wa fani mbalimbali na viongozi wengi wa ngazi tofauti," alisema.

Mradi wa ujenzi wa jengo la maabara mbili za somo la Fizikia na Jiografia, umetekelezwa kwa gharama ya Sh. milioni 99.7 fedha kutoka TASAF.

TULIKOTOKA, TULIPO & TUNAKOKWENDA

# Filamu 'Snake in the Monkey's Shadow' ilivyotikisa enzi hizo

## -Staili yake ya upiganaji inaigwa hadi leo

**Na Adam Fungamwango**






KULIKUWA na filamu nyingi sana miaka ya 1980 hadi 1990, lakini moja kati ya chache ambazo hazitoweza kusahaulika na kizazi cha miaka hiyo ni 'Snake in the Monkey's Shadow.'

Ukimuuliza mtu yoyote mzima ambaye alikuwa mtoto, kijana au mtu mzima miaka hiyo na alikuwa mpenzi wa filamu, akutajie picha tano tu za mapigano atakutajia hiyo.

Ni moja kati ya picha pendwa zaidi na athari zake zimeendelea kuonekana hadi leo hii.

Yoyote leo ambaye atataka kuigiza kupigana basi staili atakayoifanya itakuwa ni ile ya 'Snake in the Monkey's Shadow', ikiwa na maana ya nyoka kwenye kivuli cha nyani.

Atakunja mikono yake, mmoja ataupeleka juu na mwingine chini, viganja akiwa amevikunja kwa mbele vidole vikitangulia, huku mguu mmoja akiunyanyua na mwingine kubaki chini, halafu atakwambia, "nitakupiga kwa staili ya 'snake monkey shadow', utapike damu hapa."

Itakuchukua muda mrefu labda kizazi kilichozaliwa miaka 1980 hadi 1990 kiondoke juu ya uso wa dunia ndiyo filamu hii isahaulike.

Kilichoifanya iwe maarufu ni jinsi staili za mapigano zilivyokuwa zinatumika, staa wa picha hiyo akipigana na staili ya nyani na maadui wakipigana kwa mtindo wa nyoka.

Staa wa picha hiyo alikuwa akipigana na staili ya nyani aliyokuwa akiichanganya na ya mlevi hivi, lakini akakutana na vijana wawili ambao walikuwa wanapigana kwa staili ya nyoka, wakizungusha mikono yao, mmoja wakiuweka juu na mwingine chini huku vidole vyao wakivikunja kwa mbele kama kichwa cha nyoka kobra kinavyotaka kugonga mtu.

Sitoeleza picha kisa kilichopo kwenye filamu nzima, lakini ni kwamba vijana wake wawili walimsumbua sana stelingi wa filamu hiyo kwani awali hakuwa na mfumo au staili yoyote ile ya kupigana. Alikuwa anapigana kikawaida sana.

Filamu hiyo yenye dakika 100, ilitolewa na kusambazwa na kampuni ya Goldig Films LTD mwaka 1979.

Hata hivyo ilipata umaarufu miaka ya 1980 hadi miaka ya 1990 na kubaki na rekodi ya kuwa moja ya filamu maarufu, pendwa na yenye athari chanya hadi kwenye kizazi cha leo.

Ilitungwa na mtu mmoja anaitwa, Alex Gouw, ikachezwa nchini Hong Kong na kuongozwa na Cheung Sum. Aliyecheza kama stelingi kwenye picha hiyo ni John Cheung Ng Long ambaye kwenye filamu alitumia jina La Lung.

Waliocheza kama maadui kwenye filamu hiyo ambao ni wataalam wa kupigana kwa staili ya nyoka ni Wilson Tong Wai Shing aliyecheza kama Lun Chun na Charlie Chan Yiu Lam aliyecheza kama Hsia Sa.

Staa wa picha hiyo aliteseka sana kwani maadui zake hao walimkung'uta mara kwa mara kwa staili hiyo ambayo ilikuwa inamshinda kabisa.

Alionewa kiasi kwamba akaona dunia yote kama imemuinamia. Akampata mwalimu ambaye alimfundisha mapigo mengine pamoja na mazoezi ya kumfanya awe na stamina zaidi pamoja na uvumilivu.

Siku moja katika pitapita zake porini alikutana na ugomvi wa viumbe wawili. Nyoka na nyani.

Walichokuwa wakipigania hakijulikani, lakini stelingi alipoona tu vagi hili akaamua kujificha kwenye kichaka kidogo ili ashuhudie mapigano.

Alichokishuhudia ndicho kilikuja kumsaidia kwenye vita yake na maadui zake.



Nyoka alimpelekesha vilivyo nyani kwenye ugomvi ule, lakini nyani alionekana kutumia akili pamoja na staili yake ya 'kinyaninyani' kumkwepa na kumdonoa nyoka kwa mahesabu makubwa sana.

Nyoka alionekana kuwa na hasira zaidi, lakini nyani alionekana kama anapigana kwa mzaha hivi, akitumia mwili wake mnyumbulifu kukwepa, kushambulia na kuondoka haraka mara moja eneo hilo na kukaa sehemu nyingine.

Vita ile ya nyoka na nyani ilimpa somo kubwa stelingi, hasa zile staili za nyani ambazo alizikariri na kuzipigia mahesabu.

Mshindi kwenye vita ile alikuwa ni nyani, na hiyo ilimfurahisha staa ambapo alikwenda kuzifanyia mazoezi staili zote ambazo nyani alikuwa akionyesha kwenye mapigano yake na nyoka aina ya kobra.

Akafanya mazoezi kwa bidii mpaka alipohakikisha kuwa anaweza kukabiliana na adui zake. Mwisho wa siku alikutana nao.

Hawakuwa na wasiwasi kwa sababu walikuwa wanammudu. Dakika kadhaa za mapigano jamaa waligundua kuwa adui yao siyo yule tena, amebadilika na anatumia staili ya nyani.

Alifanya kama siku ile alichofanya nyani alipokuwa akipigana na nyoka. Maadui zake kama kawaida waliendelea kupigana na staili ya nyoka.

Kwa namna ya ajabu, akitumia staili aliyoiiga kwa nyani siku ile aliwasambaratisha na kuwamaliza maadui zake, akawa mshindi.

Hiyo ndiyo picha ya 'Snake in the Monkey's Shadow, iliyotikisa enzi na kubaki simulizi hadi leo.

**Tuma meseji 0716 350534**



# Putin aeleza nia ya kupeleka nafaka Afrika bure

RAIS wa Russia, Vladimir Putin ameeleza nia yake ya kupeleka nafaka katika mataifa sita ya Afrika bila malipo.

Putin alisema hayo katika mkutano kati ya Russia na nchi za Afrika mjini St Petersburg.

Katika mkutano huo Rais Putin alisema katika miezi michache ijayo wataanza kupeleka nafaka bure.

Haya yanajiri baada ya Russia kujiondoa katika makubaliano na Ukraine mapema mwezi huu.

Putin alisema kuwa nchi yake iko tayari kujaza upungufu wowote wa nafaka unaosababishwa na Ukraine.

Alisema Russia tayari kusambaza nafaka kwa nchi sita za Afrika katika kipindi cha miezi mitatu hadi minne ijayo.

Alisema, katika muda wa miezi mitatu hadi minne ijayo, itatuma tani 25,000 hadi 50,000 za nafaka kwa kila nchi.

Nchi zitakazonufaika na chakula hicho ni Burkina Faso, Zimbabwe, Mali, Somalia, Afrika ya Kati, na Eritrea.

"Tutahakikisha pia tunapeleka bure bila kulipa ada yoyote ya usafirishaji." Alisema.

# Jenerali Tchiani ajitangaza kuwa kiongozi mpya Niger

**DJMEAN,** NIGER

KIONGOZI wa mapinduzi ya kijeshi nchini Niger, Jenerali Abdourahmane Tchiani, amejitangaza kuwa Rais mpya wa taifa hilo la Afrika Magharibi.

Jenerali Abdourahmane ambaye pia anajulikana kama Omar Tchiani, aliongoza mapinduzi hayo yaliyoanza Jumatano wakati kitengo cha walinzi wa Rais alichoongoza kumkamata kiongozi wa nchi.

Hatua ya kupinduliwa kwa serikali ya kiraia, inatatiza kipindi cha kwanza cha mpito cha kidemokrasia tangu Niger ipate uhuru wake mwaka 1960.

Rais Mohamed Bazoum, bado anashikiliwa na walinzi wake na inaelezwa afya yake ni nzuri.

Hata hivyo, Wizara ya Mambo ya ndani ya utawala mpya, imepiga marufuku maandamano ya umma kufuatia watu wanaounga mkono mapinduzi hayo kuchoma moto makao makuu ya chama cha Rais aliyepinduliwa.

Polisi walirusha vitoa machozi kuwatawanya waandamanaji waliovamia makao makuu ya chama cha PNDS Tarraya,na kuishambulia kwa mawe na kuchoma moto magari.

"Maandamano ya umma kwa nia yoyote yamepigwa marufuku hadi ilani nyingine itakapotolewa.Serikali itahakikisha sheria inatekelezwa," ilisema wizara ya mambo ya ndani.

"Vitendo hivi, vilivyofanywa na watu wasioheshimu utawala wa sheria, vinajumuisha vitendo vya uharibifu na uovu mwingine havitavumiliwa," ilongeza.

Wizara hiyo imevitaka vyombo vya usalama kulinda raia na mali zao.

Aidha, Umoja wa Mataifa ulisema kuwa umesitisha shughuli zake za kibinadamu nchini Niger, baada ya wanajeshi kutangaza kumpindua Rais mteule wa nchi hiyo.

Ulisema zaidi ya watu milioni nne nchini humo kwa sasa wanahitaji msaada wa kibinadamu.

Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa Antonio Guterres, alitoa wito wa kuachiliwa mara moja na bila masharti Rais Mohamed Bazoum, ambaye anazuiliwa na maafisa wa kijeshi.

Waziri wa mambo ya nje wa Ufaransa, alisema Rais Bazoum alizungumza na Rais Emmanuel Macron siku ya Ijumaa na kumwambia kwamba sehemu aliyohifadhiwa inafikika na yuko na afya njema.

Baadhi ya wafuasi wa kundi la waasi nchini Niger, walifanya maandamano nje ya Bunge la taifa hilo huku wakibeba bendera za Russia.

Russia imeyaita mapinduzi hayo kuwa ni hatua mbaya ya kupinga katiba.

Nchi mbalimbali zimetoa wito wa kuachiliwa huru kwa Rais Bazum, ambaye anashikiliwa na wapiganaji hao hadi sasa.

**BBC**

# Mahakama Kenya yaruhusu serikali kukusanya kodi tata

**NAIROBI.** KENYA

MAHAKAMA ya Rufani ya nchini Kenya, imeruhusu sheria ya nyongeza ya kodi inayoleta utata inaweza kutekelezwa.

Sheria hiyo imesababisha maandamano kutoka kambi ya upinzani katika miezi kadhaa yaliyoifanya nchi hiyo kukosa usalama wa kutosha.

Katika maandamano hayo watu 30 walifariki dunia na wengine kujeruhiwa.

Wakosoaji wa sheria hiyo walisema itakapoanza kufanya kazi itapandisha gharama ya maisha kwa mamilioni ya watu wa ngazi ya chini. Sheria hiyo iliidhinishwa na Rais William Ruto mwezi Juni, inalenga kupadisha ushuru wa VAT kwa bidhaa za mafuta kutoka asilimia 8 hadi 16.

Pia itaongeza kodi ya nyumba kwa asilimia 1.5 utakaolipwa na waajiri na waajiriwa.

Uamuzi wa mahakama ya rufani unaipa hazina idhini ya kuanza kukusanya kodi hiyo mpya.

Huenda uamuzi huo ukazua maandamano zaidi ya upinzani.

Katika hatua nyingine, huduma za kawaida zimerejea kwenye mtandao wa serikali wa Kenya, unaojulikana kama e-Citizen, baada ya kusitishwa kutokana na jaribio la udukuzi.

Raia wa nchi hiyo walikosa huduma ya ununuzi wa umeme, kufanya miamala kwa njia ya simu, huduma za benki za kidigitali na huduma za serikali zinazotolewa kwa njia ya kidigitali kupitia e-Citizen. Shambulio hilo la mtandao lililolenga taasisi za umma na za kibinafsi, lilidaiwa kutekelezwa na watu wanaojiita Anonymous Sudan.


## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**NDASKOY ITAELY MUNISI,**

Anatangaza kupotea kwa kadi mbili za pikipiki, ya kwanza yenye namba za usajili MC 185 BFK aina ya GSM, Chassis No. LV7MKA404-FA905580, Engine No. 162FMJ1506063042. Ya pili aina ya BAJAJ BOXER yenye namba za usajili MC 131 CMW, Chassis No. MD2A21BY5LWK92330. yeyote atakaeziona atoe taarifa Kituo chochote cha Polisi.

Taarifa ya Polisi: **DOD/DOD/RB/165543/2023.**


**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**J/PCF/54**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(MCA/63)**
**MAHAKAMA YA MWANZO : MANGAKA**
**WILAYA YA NANYUMBU**
**MADAI NAMBARI: 43 YA 2023**
**MDAI :CONSTANTINO FAUSTINO MTITU**
**MDAIWA: HAWA SAIDI HASSANI**

**KWA:(1)....................................**
**:(2)....................................**

Kwa kuwa mdai /wadai ameleta /wameleta madai yake /yao kwamba (eleza hapa Habari za madai) **UFIKE MAHAKAMANI BILA KUKOSA KUJIBU MADAI YAKO YA FEDHA KIASI CHA TSH 27,500,000/= MILLIONI ISHIRINI NA SABA NA LAKI TANO**

Kwa hiyo unahitajiwa/mnahitajiwa kuhudhulia binafsi katika Mahama hii ya mwanzo ya Mangaka Tarehe 07 mwezi, 08 2023 sa 8:00 asubuhi

Kwa kujibu madai hayo kwakua siku hio ni siku ya kukata shauri hilo / lazima kuleta mashahidi wako / wenu na hata zote zinazohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea katika shauri hilo

**ANGALIZO:** Kama hukuhudhuria/hamkuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu Mahakama ikithibitisha kama umepokea /mmepokea kuitwa shaurini hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa / mmeshindwa.

Hati hii imetolewa kwa amli yangu na chapa ya Mahakama hii leo **tarehe 02 mwezi wa 07 2023**

HAKIMU MAHAKAMA YA MWANZO MAHAKAMA YA MWANZO MANGAKA


## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**SAIMON PETER BINDE,**

Anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya TOYOTA MARK II, Yenye no za usajili T 829BEZ, CHASSIS NO GX1106103262 Yeyote atakaeiona atoe taarifa Kituo cha Polisi.

TAARIFA YA POLISI: **MAN/SIM/RB/225962/2023**


**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 86/2023**
**In the matter of the Estate of the NAIDA SILLAH NGOGO of NDACHI within Dodoma Region.**
**And**
**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR PROBATE WITH WILL ANNEXED BY**
**SHARMA MWINYIKHERI BARUSHI**
**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules GN 369 of 163)**

All persons claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant for probate is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before 17 Day of AUGUST 2023.

Date at Dodoma this 22rd day of July 2023.

RESIDENT MAGISTRATE I/C DODOMA DISTRICT

RESIDENT MAGISTRATE

**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA KIGOMA**
**MAHALI: KIGOMA**
**MAOMBI NA. 45 MWAKA 2023**
**ELIAS RICHARD KAFUKU...........MWOMBAJI**
**DHIDI YA**
**MOSHI KAKOSO.................MJIBU MAOMBI**
**KUITWA SHAURINI**

**KWA: MOSHI KAKOSO**

Fahamu kwamba shauri hili limepangwa kutajwa/kusikilizwa tarehe 01 Mwezi 08 Mwaka 2023 saa 2:30 asubuhi/mchana mbele ya Mh. MWINYI Mwenyekiti wa Baraza. Hivyo unaamriwa kuhudhura mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa.

AMRI hii imetolewa kwa mkono wangu na Lakiri/Muhuri wa Baraza hili leo tarehe 25 Mwezi 07 Mwaka 2023.

MWENYEKITI

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**HATI YA KIAPO**

Mimi FATUMA HASSANI WASIA, mtu mzima mwenye akili timamu, mkazi wa Mtaa wa Duga kata ya Duga katika Halmashauri ya Jiji la Tanga, bila kushawishiwa na mtu yeyote naapa kama ifuatavyo:-

- Kwamba, FATUMA HASSANI WASIA na MWANAUWANI HASSANI WASIA ni wamiliki wa Offer ya kiwanja namba "87" kitalu "Q" kilichopo Duga katika Halmashauri ya Jiji la Tanga.
- Kwamba, Offer Milki ya kiwanja hicho imepotea na nimefanya juhudi za kutafuta bila mafanikio.
- Kwamba, kwa kiapo hiki naomba idara ya ardhi na mipango miji wilaya ya Tanga inipatie Offer nyingine ya umiliki wa kiwanja hicho.

UTHIBITISHO

Mimi FATUMA HASSANI WASIA nathibitisha kuwa yot niliyoyasema hapo juu kuanzia aya ya 1-3 ni kweli tupu kwa jinsi nijuavyo na kwa mujibu wa sheria ya viapo (The Oaths and Statutory Declaration Act.Cap.34 R;e 2019).

Imethibitishwa hapa Tanga
Tarehe....
Mbele Ya....
Anwani....
Cheo....
Sahihi....

Sahihi ya Muapaji


## KUPOTEA KWA OFA YA KIWANJA

**JOYCE JOSEPH CHILONGA**

**Anatangaza kupotelewa na OFA YA KIWANJA chenye utambulisho wa PLOT No.809/10 BLOCK 'A' TUNGI (MGENI HIJA NGATOLUWA),**

**Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha polisi MOR/MOR/RB/248021/2023.**



## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

Ndugu **KHAMISI RAMADHANI SHIMBO** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya TOYOTA COASTER yenye namba za usajili T.211 BPQ.

Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.Taarifa

**Polisi: TAN/RB/252990/2023.**


**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika mahakama ya mwanzo ya wilaya ya TEMEKE**
**Kituo cha JUMUISHI mkoa DAR ES SALAAM**
**Usimamizi wa Mirathi na 1088/2023**
**Katika shauri la mirathi ya Marehemu:**
**NDEGELA MANENO MBUNGI**
**KATIKA SHAURILA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA :**
**REHEMA DOMONICK NA MANENO MAMBO MBIGI**

**TANGAZO**
**(kanuni ya tano (2) ya kanuni za usismamizi wa mirathi mahakama za mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote /maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu ,wanahalikwa kuja na kuhudhulia katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 18 mwezi 08 mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo

**Zingatia :**

Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa marehemu anaweza kuuleta mahakamani kukaguliwa

*Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani na waweza kukaguliwa

*marehemu hakuacha wosia

* futa isio husika

Imetolewa leo tarehe 27 mwezi wa 7 mwaka 2023

HAKIMU

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**SOLLAR JIMMY MWAKYUSA** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI **T.942 ASQ.**YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHO KARIBU.TAARIFA YA POLISI **MBE/MBE/RB/253222/2023**

## KUPOTEA KWA VYETI



**JOSEPHINE EMMANUEL KAHENSA** anatangaza kupotelewa na vyeti, cheti cha chakuhitimu kidato cha nne index No. S.4565-0012 GILI SECONDARY SHOOL mwaka 2017, na Kidato cha Sita index No S.0256-0524 HURUMA GIRLS' SECONDARY SHOOL mwaka 2020. vilivyotolewa na Baraza la mitihani la Taifa.

Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

Taarifa polisi: DOD/DOD/RB/243759/2023

Taarifa ya polisi DOD/DOD/RB/243761/2023

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

HAMADI HAMISI MAKURA anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki yenye namba ya usajili T 776 AQU – aina ya Honda. Chassis namba 156FMI6E050416. Engine namba LXYPOLD26008655. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: ARU/ARU/B/252252/2023.

**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**MASJALA NDOGO YA TEMEKE**
**(TEMEKE KITUO JUMUISHI HUDUMA ZA MAHAKAMA MIRATHI NA NDOA)**
**MIRATHI NAMBA 68 YA MWAKA 2023**
**MAOMBI YA BARUA ZA USIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMU**
**MICHAEL NYARI YONA**
**LILIAN GODFREY KAMUKALA.....MUOMBAJI**

### TAARIFA YA KAWAIDA

**(Kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua za usimamizi wa mirathi kwa mwombaji hapo juu.

Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 22 mwezi wa 8, 2023 saa 02:00 asubuhi.

Imesainiwa Dar es salaam, leo tarehe 20 mwezi wa 07, 2023.

NAIBU MSAJILI

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**FLORENCE KYEUPE SHAYO** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye usajili namba: **T457 ACQ,** CHASSIS NAMBA: **YN566001871** na ENGINE NAMBA: **2Y0223915.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA: **ARU/ARU/RB/213747/2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**SIFA WILIAM FRED** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye usajili namba **T 141 DPW.** kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA: **ARU/ARU/RB/253409/2023**

**IN THE DISTRICT COURT OF KOROGWE**
**AT KOROGWE**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO .......21.....OF 2023**
**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE BLANDINA DOMINICK KIVUGO**
**AND**
**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION**
**BY JOHN JAMES KIVUGO**
**(Rule 75 of probate Rules GN 369 OF 1963)**

**ALL PERSON** claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named petitioner

Objections to the grant should be filed on or before the 24th day of August 2023

**Dated at Korogwe this 24th day of July 2023**

RESIDENT MAGISTRATE
KOROGWE

**HALIMASHAURIYA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

| | |
|---|---|
| Simu Nambari 275616 | Ofisi ya Hakimu Mkazi Mfawidhi |
| Email: haido@judiciary.go.tz | Mahakama ya Mwanzo Bomang'ombe |
| Tovuti:http//wwwjudiciary.go.tz | 12 Barabara ya Ardhi Samunge |
| Unapojibu tafadhali taja | S.L.P 88. |
| Kumb:Na: TALAKA NO.11/2023 | 25316 MUUNGANO-HAI |
| | Tarehe 24/7/2023 |

**SHAURI LA TALAKA NA. 11/2023**

**MDAI : HOLLYNESS SIMBO MWASHA**

**MDAIWA : GEORGE CHRISTONFOO KWEKA**

**KWA GEORGE CHRISTONFOO KWEKA**

**POPOTE ULIPO TANZANIA BARA NA VISIWANI**

Shauri tajwa hapo juu imefunguliwa katika Mahakama ya mwanzo Bomang'ombe. Unatakiwa kuhudhuria hapa Mahakamani tarehe 7/8/2023saa 08:30 asubuhi fIka bila kukosa usipofika Mahakamani shauri litasikilizwa upande mmoja.

HAKIMU MKAZI MFAWIDHI
MAHAKAMA YA MWANZO BOMANG'OMBE
HAI

## KUPOTEA KWA CHETI



**ZACHARIA THOMAS MUNISI** anatangaza kupotea kwa cheti chenye index namba: **S.4209/0026** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **FOUNTAIN OF HOPE CHRISTIAN SEMINARY** mwaka 2020. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **DAR/CHU/RB/230283/2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**EDWIN ENOSY SWALLE** anatangaza kupotelewa na kadi ya Gari yenye namba za usajili **T102DMW** aina ya **TOYOTA IST.** Chassis No. **NCP650029286,** Engine No. **1NZB271371.**Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi Taarifa ya polisi **DOD/DOD/RB/252239/2023**

**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**MASJALA NDOGO YA TEMEKE**
**(TEMEKE KITUO JUMUISHI HUDUMA ZA MAHAKAMA MIRATHI NA NDOA)**
**MIRATHI NAMBA 68 YA MWAKA 2023**
**MAOMBI YA BARUA ZA USIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMU**
**MICHAEL NYARI YONA**
**LILIAN GODFREY KAMUKALA.....MUOMBAJI**

### TAARIFA YA KAWAIDA

**(Kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua za usimamizi wa mirathi kwa mwombaji hapo juu.

Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 22 mwezi wa 8, 2023 saa 02:00 asubuhi.

Imesainiwa Dar es salaam, leo tarehe 20 mwezi wa 07, 2023.

NAIBU MSAJILI

**WINDING UP THE COMPANY FROM REGISTRY DUE TO NIL BUSINESS ACTIVITIES**

**THE COMPANY ACT, 2002**
**AGRO DODOMA LIMITED**
**P.O.BOX 2791, DODOMA**

**A MEMBERS MEETING HERD ON THE 01 MARCH 2023, AT DODOMA**

| ATTENDANCE | SIGNATURE |
|---|---|
| 1. GUDMUND NILSEN | |
| 2. RUKIA SHABANI JUMA | |
| 3. DANIEL CHIDYAKA CHILONWA | |
| 4. RICHARD SHABULOOMA LWOGA | |
| 5. MARIA BELESU LEONARDI | |
| 6. FAUDHIA HASHIM YASSIN | |
| 7. SHAMSA NASSORO MUHAMEDY | |

At the meeting of the Board of the Company held on **1st March 2023** in Dodoma. The Board of Directors enormously resolved to have **AGRO DODOMA LIMITED** in Tanzania, Dodoma of **P.O.BOX 2971** to be strike off according to **Company Act 202, Section 400sub section 3.**

**This resolution reads, "The Members of AGRO DODOMA LIMITED approve the voluntary winding up of the company according to Companies act 2002 Chapter III,333, (I)(b), Due to nil carry out of the activities."**

Having no other agenda to transact, the meeting was called to halt at 14:30p.m. by chairman.

**GUDMUND NILDEN** — **Chairperson**

**RICHARD SHABULOOMA LWOGA** — **Secretary**

## MNADA WA HADHARA

**JOFORTE AUCTION MART COMPANY LTD** Kwa niaba ya Benki ya CRDB, Tunatoa taarifa kwa wadaiwa/wadhamini wafuatao kulipa madeni yao yote wanayo daiwa na benki hiyo kuwa ndani ya siku kumi na nne kuanzia tarehe ya tangazo hili, Iwapo watashindwa kufanya hivyo tutauza kwa njia ya mnada wa hadhara dhamana zao kama inavyo onesha kwenye jedwali hapa chini.

| S\N | JINA LA MDAIWA\MDHAMINI | DHAMANA MAHALI ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|
| 1. | HEKIMA MWASIPU | DHAMANA ILIYOPO KWENYE KIWANJA KISICHOPIMWA ENEO LA KINONDONI SHAMBA, WILAYA YA KINONDONI. | 15\08\2023 kuanzia saa 4:30 asubuhi na kuendelea. |
| 2. | MATILDA NICHOLAUS CHUWA | DHAMANA ILIYOPO KWENYE KIWANJA KISICHOPIMWA ENEO LA MSUFINI-CHAMANZI, WILAYA YA TEMEKE. | 17\08\2023 kuanzia saa 4:30 asubuhi na kuendelea. |
| 3. | TWAHILI BAKILI SALUM | DHAMANA ILIYOPO KWENYE KIWANJA KISICHOPIMWA ENEO LA MAJENGO, WILAYA YA TANDAHIMBA. | 22\08\2023 kuanzia saa 4:30 asubuhi na kuendelea. |
| 4. | TWAHILI BAKILI SALUM | KIWANJA NA 141, KITALU 'A' ENEO LA POLISI, MANISPAA YA MTWARA | 24\08\2023 kuanzia saa 4:30 asubuhi na kuendelea. |

**Masharti ya Mnada.**

1. Dhamana itauzwa kama ilivyo.
2. Mnunuzi atalazimika kulipa 25% ya bei ya nyumba au kiwanja papo hapo baada ya mnada kumalizika na 75% itakayobaki italazimika kulipwa ndani ya siku 14.
3. Ikiwa mnunuzi atashindwa kutimiza sharti lolote la mnada kuhusiana na malipo ya awali, hatarudishiwa pesa yoyote aliyokwishailipa.
4. Gharama zote za kubadili hatimiliki ni za mnunuzi
5. Gharama za umiliki na kumtoa mwenye dhamana ni za mnunuzi
6. Kwa mawasiliano zaidi; tupigie simu no. **0659706393 / 0734232220/ 0717935186(Revacco)**

## MNADA WA HADHARA

Kutakuwepo na mnada wa hadhara wa kuuza dhamana za wadaiwa sugu. Mnada utaendeshwa na madalali tajwa hapo chini kwa idhini ya **Tujijenge Tanzania Financial Service Ltd** kama ilivyotangazwa gazetini:-

| Mdhamini/ Mdaiwa | Dhamana/ Mahali ilipo | Tarehe ya mnada/ Dalali |
|---|---|---|
| Juma Chiza Rubabwa/Mapinduzi Kivwangi | Nyumba- Kizuiani Mbagala. | 08.09.2023 - SEPCO Debt collector |
| Mapinduzi Wilson Kivwangi | Nyumba – Mtaa wa Mogo Kipawa DSM | 22.09.2023 - SEPCO Debt collector |
| Gregory Isdory Wenceslaus | Plot – Kimara-King'ong'o -DSM Plot- Kibamba Mkuranga | 15.08.2023 - White miracles 15.08.2023 |
| Bernard Daud Nkeyemba | Nyumba- Madale DSM | 16. 08.2023 DENNESTO Investment Ltd |
| Steven Samwel Dumba/ Bernard Nkeyemba | Nyumba- Ferry Kigamboni | 21. 08.2023 DENNESTO Investment Ltd |
| Abdul Hashim Said | Nyumba- Mbondole (DSM) | 25.08.2023 Dennesto Inv. Ltd |
| Naomi Joseph Wambura | Nyumba- Mbondole (DSM) | 25.08.2023 Dennesto Inv. Ltd |
| Yahaya Khalid Ally | Nyumba- Kihonda Morogoro | 18.08.2023 Diamond Credit |

**Masharti Mengine:**

Minada yote itafanyika mahali dhamana zilipo kuanzia saa nne asubuhi. Mteja atalipa 25% siku ya mnada, 75% atalipa ndani ya siku 14, akishindwa kulipa 25% iliyolipwa hairudishwi. Gharama za kuona, kukagua, kuhamisha umiliki, kumtoa mdaiwa/mpangaji ni juu ya mnunuzi.

**Mawasiliano piga: SEPCO- 0715683777; White Miracles-0782359900 DENNESTO-0658896226; Diamond; 0789455445**

## KURUDIA MNADA WA HADHARA

**RAISSA COMPANY LIMITED** tunatangazia umma kuwa kutakuwepo na marudio ya mnada wa hadhara wa kuuza dhamana ya mdaiwa sugu kama ilivyoonyeshwa kwenye jedwali hapo chini. Mnada itaendeshwa kwa idhini tuliyopewa na **Tujijenge Tanzania Financial Service Ltd** kama ilivyotangazwa gazetini:-

| Mdaiwa | Dhamana/ Mahali ilipo | Tarehe ya mnada | Dalali |
|---|---|---|---|
| Biswaro Zebedayo Msase | Nyumba- Ipo Mtaa Mloganzila- Kwembe - Dsm | 04/08/ 2023 | **RAISSA CO. LTD** |

**Masharti Mengine:**

Minada itafanyika mahali dhamana zilipo kuanzia saa nne asubuhi. Mteja atalipa 25% siku ya mnada, 75% atalipa ndani ya siku 14, akishindwa kulipa 25% iliyolipwa hairudishwi na mnada utarudiwa tena. Gharama za kuona, kukagua, kuhamisha umiliki, kumtoa mdaiwa/mpangaji ni juu ya mnunuzi.

**Mawasiliano piga: RAISSA Company Ltd: 0652113262/ 0757433333**

*Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0677020701*

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# HADITHI

MBWA mmoja wa jirani wa maeneo ya Kinondoni Msisiri, alionekana kuvutiwa na kiroba kilichotupwa upenuni mwa nyumba moja. Ni moja kati ya viroba ambavyo hutupwa usiku au alfajiri na vijana wanaokusanya taka kwenye nyumba za watu na kupewa ujira kidogo. Wao badala ya kwenda kutafuta maeneo ya kutupa, hupita vichochoroni na kama hajaonekana anautupa mzigo na kuendelea na safari yake. Ilitokea kwenye nyumba moja huko na mbwa huyo alipouvuta, viungo vya mwili wa binadamu vilianguka. Majirani wa kwanza kuona walipiga kelele na watu wakajazana. Wakinamama wakiangua vilio. Viungo vilihifadhiwa kwa kufunikwa. Polisi walianza msako. Kwa kuanzia tu wakaanza kuwakamata wazoa taka na waokota chupa za kwenda kuuza, wote wa maeneo hayo na jirani wanaofahamika tayari kwa mahojiano na uchunguzi, wakihisiwa kuwa huenda mmoja wao au zaidi kahusika na mauaji. Ni maiti ya nani? Na Muuaji ni nani? Fuatilia mwanzo hadi mwisho kujua mkasa mzima ulivyokuwa.

## MAITI KWENYE KIROBA-19

**Na Adam Fungamwango : (0716 350534)**

"Alikuwa na nani?"

"Alikuwa na watu wawili."

"Walikwambia wanakwenda wapi na kufanya nini?"

"Hawakuniambia, ila walikuwa na mzigo."

"Mzigo wa nini?"

"Sikuwauliza, ila walionekana kama wamenunua mzigo hivi, wakauweka kwenye buti, nikawapeleka hadi Magomeni, mimi nikarudi zangu."

"Walikupigia simu kutoka uwanja wa ndege?"

"Ndiyo, na kwa sababu mimi huku napafahamu, jamaa aliniambia atakuwa madukani ananunua mzigo, hivyo nisiende nyumbani kwake tutakutana kituoni."

"Ilikuwa saa ngapi?"

"Saa tano ya usiku yaani kama saa hizi."

Ingawa dereva alikuwa anajibu kwa kifupi kile tu anachokifahamu, lakini alikuwa hafahamu kuwa majibu yote aliyokuwa akijibu yalikuwa muhimu mno kwa Eddy, yalimuongezea vitu vingi ambayo vilionekana kumpa mwanga wa tukio zima la mauaji ya Tessy.

"Sasa sikiliza nikwambie. Usimwambie mtu yoyote kuhusu jambo hili. Kuanzia nilipokukodisha hadi hapa tulipofika. Na nasema hivi kwa usalama wako. Yoyote utakayemwambia basi utakuwa ndiyo mwisho wako. Na siyo kama mimi nitakuua, huyo au hao utakaowaambia watakumaliza. Kuwa mwangalifu, mimi ni mtu mzuri tu. Yoyote atakayekusumbua, piga simu namba hii." Akampa dereva namba ya Maria mfanyakazi wa pale pale uwanja wa ndege.

Eddy aliteremka maeneo ya Kipawa, akamlipa dereva mara mbili ya pesa ambazo alitakiwa kumlipa.

Dereva alishangaa. Hakujua amuweke kwenye fungu gani.

"Mbona kama ni jambazi, au mtu mbaya na katili? Halafu mbona kama ni askari au mtu mzuri mwenye huruma?"

**********************************

"Niambie Inspekta Frank." Eddy alianza kwa kumsalimia mara tu aliponyanyua simu yake ya mkononi.

"Safi tu za huko na habari za kazi."

"Kazi inaendelea vizuri na leo hii saa 12, nataka nikupeni zawadi ndogo tu."




"Zawadi gani tena hiyo?" Inspekta Frank alishtuka.

"Waambie wale vijana wako ambao nilikuambia wasimame kwanza kazi hii ya kumpeleleza muuaji wa Tessy, waende pale Lango la Jiji Magomeni saa 12:00 jioni wakamchukue mtu fulani hivi. Huyo mtu ni muhimu sana kwa ajili ya kumpata yule jamaa yetu tunayemhitaji."

"Okay, ni Sajenti Moses na Koplo Ben ambao ndiyo walioianza kesi hii kabla ya kukukabidhi wewe."

"Sawa, ila wanachopata kukifanya ni kumkamata tu na kumleta kwenye ofisi yangu, nina watu ambao watamuuliza maswali, kama atakataa wanamtia msukosuko kidogo, halafu akikubali wataniletea kwa ajili ya mahojiano."

"Ina maana tayari kuna mtu umeshamhisi au kumfahamu?"

"Siyo kumhisi, tayari muuaji nimeshamfahamu." Eddy aliongea kwa sauti ilionyesha kuwa ana uhakika na anachokisema.

"Sasa kwa nini tusiende kumkamata huyu muuaji ili wananchi wafurahi na serikali nzima ifurahi, upewe na tuzo." Inspekta Frank akachombeza.

"Nina tuzo kibao ndani, ninayoitaka ni ile inayotolewa na wananchi na kwa swali lako kuwa kwa nini asikamatwe sasa hivi ni kwamba tukishindwa tu kumkamata sasa hivi, basi atatushinda mahakamani mchana kweupe!"

"Kwa nini Eddy, ni mjanja sana, au imekaaje hiyo?"

"Kwa ujanja kweli ni mjanja, amejitahidi mno kufuta nyayo kila anapopita, ila kwa bahati mbaya tu amekutana na mimi. Ninachokipigania sasa hivi mimi siyo kumkamata, kufanya hivyo naweza kwenda mimi mwenyewe nikamchukua au nikakwambia utume vijana wako wamtie mbaroni. Mbona huyu mwingine nimekwambia nendeni mkamkamate mliniletee?"

"Sasa tatizo ni nini Eddy?"

"Ukidili na watu kama hawa jitahidi kupata ushahidi. Huo ndiyo muhimu sana, unaweza kuchukua muda mrefu na nguvu nyingi kuwakamata wahalifu lakini mahakamani wakakuachia mtupu. Mtu kaua kabisa au kafanya uhalifu, lakini kwa sababu umefanya pupa kumkamata unakosa ushahidi na yeye anaachiwa huru, mnakuwa mmefanya kazi bure, ni kama vile hamjafanya kitu, mmetumia muda wetu mwingi na rasilimali za taifa kwa hasara." Akajibu Eddy kwa sauti iliyopenya vema kwenye masikio ya Inspekta Frank.

"Sasa huyu ambaye atakwenda kukamatwa leo jioni ni mmoja wa washirika au?"

> **"Sasa huyu ambaye atakwenda kukamatwa leo jioni ni mmoja wa washirika au?"**

"Na siyo yeye, yaani mkiniletea, itabidi atusaidie kwanza kumpata mwenzake. Hawa wakitupa ushirikiano wanaweza kuwa mashahidi wazuri au kuwa na ushahidi mzuri."

"Vizuri bwana Eddy, inavyoonekana kazi bado kidogo tu imalizike."

"Tuombe Mungu, lakini inavyoonekana imekwisha hii, watu wajiandae tu kumjua muuaji halisi."

**********************************

Eddy aliamua mtu huyo akamatwe baada ya kupigiwa simu kutoka kwa dereva taxi aliyekuwa naye wiki iliyopita na kumpeleka mpaka Ukonga Banana.

Baada ya kupewa namba ya Maria, dereva yule hakutaka kumchukulia Eddy kama jambazi, bali ni mtu mwema na anataka kufanya kitu chema.

Pamoja na kwamba alimteka kwa kumuwekea bastola shingoni, dereva yule aliona kama ilikuwa ni mbinu tu aliyoitumia kwani angetumia muda mwingi na mlolongo mrefu mpaka akubali. Ni kweli asingeweza kukubali kiurahisi hivyo.

Kitendo cha kuachiwa huru bila kudhuriwa, kulipwa mara mbili ya kazi aliyoifanya kutoka Uwanja wa Ndege wa Julius Nyerere, kumpeleka Kawe, halafu kumrudisha hadi Ukonga Banana na kutoka huko mpaka Kipawa, licha ya kumjulisha hesabu ya woga, lakini yeye aliamua kulipa mara mbili yake, kilimuonyesha hakuwa mtu mbaya.

Pia alimtahadharisha kuwa asimwambie yoyote tukio lile na siyo kwa sababu ya abiria yule kuogopa, ila kumhofia yeye kama dereva kuuawa au kufanyiwa kitu kibaya na mtu yoyote ambaye angeweza kumuuliza tukio hilo au kumwambia.

Hapo alihofia kuwa jambo lile lingeweza kufika kwa watu ambao wana uhusiano na tukio alilolifanya.

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

# MANYAMA KUIKOSA YANGA NGAO YA JAMII

**Na Shufaa Lyimo**

AZAM FC imepata pigo kuelekea kwenye michezo ya Ngao ya Jamii baada ya beki wake Edward Manyama kuumia akiwa kwenye kambi ya timu hiyo nchini Tunisia na imethibitisha atakosa michezo hiyo.

Azam imepangwa kucheza na Yanga kwenye mchezo wa Ngao ya Jamii Agosti 9 na kama watafanikiwa kushinda mchezo huo watakutana na mshindi wa mchezo kati ya Simba na Singida Fountain Gate katika mchezo wa mwisho wa kuamua bingwa wa Ngao ya Jamii kwa msimu huu.

**Akizungumza na gazeti la Nipashe kutoka Tunisia, Daktari wa timu hiyo Mwanandi Mwankemwa alisema mchezaji huyo atakaa nje kwa muda wa wiki mbili akiwa chini ya uangalizi wa daktari.**

"Manyama aliteguka bega juzi tulipokuwa tunacheza mchezo wa kirafiki atakaa nje siku hizo mpaka hapo atakapokaa sawa, hawezi kuwahi michezo y aNgao ya Jamii," alisema Mwankemwa.

Alisema tayari mchezaji huyo ameanza kupatiwa matibabu na kwa sasa hali yake inaendelea kuimarika tofauti na ilivyokuwa hapo awali kwani walidhani amevunjika mkono.

"Naomba watanzania pamoja na mashabiki wetu wasiwe na wasiwasi juu ya mchezaji huyo yupo kwenye uangalizi mzuri tulifikiri alivunjika baada ya kufanyiwa uchunguzi amebainika ameteguka tu," alisema Mwankemwa.

Aidha, alisema ukimuondoa Manyama hakuna mchezaji mwingine mwenye majeraha makubwa na wote wapo kwenye hali nzuri wakiendelea na mazoezi.

Manyama aliumia wakati Azam ilipokuwa ikicheza mchezo wa kirafiki na dhidi ya Stade Tunisie mchezo ambao hata hivyo ulivunjika dakika ya 60.




Watoto wakicheza mpira katika viwanja vya Jakaya Kikwete jijini Dar es Salaam kama walivyokutwa na mpiga picha jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Shime azihofia Z'bar, Uganda*

**Na Saada Akida**

KOCHA wa timu ya taifa ya Tanzania ya wasichana chini ya miaka 18, Bakari Shime amesema bado ana kibarua kigumu kwenye michezo yake miwili dhidi ya Zanzibar na Uganda ya mashindano ya kuwania ubingwa wa michuano ya soka inayoandaliwa na Baraza la mchezo huo la Afrika Mashariki na Kati (CECAFA ).

Tanzania ambayo ni mwenyeji wa mashindano hayo ilianza vizuri kwenye michezo yake miwili baada ya kuibuka na ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Burundi mwanzoni mwa wiki na juzi pia kufanikiwa kupata ushindi kama huo dhidi ya Ethiopia.

Akizungumza na Nipashe muda mfupi baada ya kumalizika kwa mchezo dhidi Ethiopia, Shime alisema anawapongeza zaidi wachezaji wake kwa kupambana na kufuata maelekezo yake na kupelekea kupata ushindi huo.

"Kipindi cha pili kilikuwa kigumu kwetu kwa sababu ya umakini wa Ethiopia, lakini tumelinda bao na kuongeza bao ligine, ukiangalia timu imecheza tofauti na mchezo wetu wa kwanza, wachezaji wamefanya kazi nzuri sana," alisema Shime.

Hata hivyo alisema pamoja na ushindi katika michezo hiyo miwili, bado ana kibarua kigumu kwenye michezo miwili iliyobakia dhidi ya Zanzibar na Uganda.

"Mechi hii bado haijatupa wepesi kwenye michezo inayofuata, bado tuna michezo miwili ambayo kwa kweli si mechi nyepesi," alisema Shime.

Aliongeza katika michezo hiyo miwili iliyobakia hataangalia matokeo ya mpinzani wao kwenye mechi zilizopita badala yake watapambana kupata ushindi.

"Mechi dhidi ya Zanzibar sio rahisi, tunahitaji kupambana kushinda mechi hiyo baada ya hapo tunaenda kupanga jinsi ya kumalizia hatua hii dhidi ya Uganda, katika mashindano haya niliofia sana timu ya Ethiopia lakini umeona tumefanikiwa kupata matokeo ," alisema Shime.

Alisema hakuna mechi rahisi na haichukulii Zanzibar kama timu kibonde kwa sababu mpira ni mchezo wa makosa wakiwadharau wanaweza wakapata matokeo ya kushangaza.

Kuhusu uwezekano wa kutwaa ubingwa wa mashindano hayo, Shime, alisema malengo yao ni kuona wanabakiza kombe hilo katika ardhi ya Tanzania hivyo watapambana katika kila mchezo kuweza kupata ushindi.

## Wavu taifa kujulikana leo

**Na Shufaa Lyimo**

KOCHA wa timu ya taifa ya mpira wa Wavu, Alfred Selengia leo anatarajiwa kutangaza majina ya wachezaji watakaounda timu hiyo kwa upande wa Wanawake na wanauame kwa ajili ya mashindano ya Mataifa ya Afrika yatakayofanyika katika nchi mbili tofauti.

Mashindano ya Afrika kwa timu za taifa za wanaume yanatarajiwa kufanyika Misri Septemba mwaka huu wakati yale ya wanawake yatafanyika Cameroon mwezi ujao

Akizungumza na gazeti la Nipashe jana, Selengia alisema baada ya kutangaza vikosi hivyo moja kwa moja wataanza kambi kujiandaa na mashindano hayo.

"Jumapili (kesho) nitatangaza timu ya Taifa ya Wanaume na Wanawake ambazo zitaingia kambini kwa ajili ya kufanya maandalizi kuelekea katika mashindano hayo, muda umetutupa mkono sana hivyo baada yakutangaza tu tutaingia kambini kujiandaa," alisema Selengia.

Alisema wachezaji atakaowatangaza wote wamepatikana kwenye michuano ya Ligi ya Taifa ya mchezo huo kwenye mzunguko wa kwanza na wa pili inayofikia tamati kesho viwanja vya Gwambina, jijini Dar es Salaam.

Alisema amefurahishwa na viwango vilivyoonyeshwa na kila timu ambapo ameweza kuchagua wachezaji wa timu ya taifa wenye uwezo m kubwa.

"Tunashukuru kwa sasa mchezo huu wa wavu umeinuka tena ukilinganisha na miaka ya nyuma, kwa sasa umekuwa na hamasa kubwa," alisema kocha huyo.

Ligi hiyo ya taifa inayofika tamati leo ilishirikisha klabu kutoka mikoa ya Tanzania bara na Zanzibar.

## Mashindano baskeli taifa kuanza leo

**Na Abdallah Mataka**

MASHINDANO ya taifa ya mbio za baiskeli yanaanza kufanyika leo jijini Arusha yakiwa na lengo la kusaka timu ya taifa ya mchezo huo.

Akizungumza na Nipashe jana, Mwenyekiti wa Chama cha mchezo huo nchini (CHABATA), Godfrey Muhagama alisema tayali washiriki kutoka mikoa yote wamewasili na maandalizi yote ya mshindano hayo yamekamilika .

"Kwa ujumla kila kitu kimekamilika kuelekea katika mashindano hayo ikiwemo usalama wa njia zitakazotumiwa na wachezaji zote zipo vizuri"alisema Muhagama.

Muhagama alisema lengo kubwa la mashindano hayo ya siku mbili ni kwa ajili ya kuchagua wachezaji wa kike na wakiume watakaounda timu ya taifa itakayowakilisha nchi kwenye mashindano ya kimtaifa.

"Kwenye haya mashindano hapa ndio mahali ambapo tunapata timu ya Taifa ya baiskeli ambayo itatuwakilisha katika mashindano yote ya kimataifa,"alisema Muhagama.

Aidha amewataka wadau pamoja na wadhamini kujitokeza kwa wingi kuisaidia CHABATA ili kiweze kupiga hatua kuendelea kwenda mbele zaidi katika kuutangaza mchezo huo hapa nchini.

## ZISIKUPITE

### KANE NA BAYERN

VIONGOZI wa Bayern Munich wamesafiri kuelekea London kwa mazungumzo mapya na Tottenham Hotspur kuhusu ofa ya pauni milioni 86 ya kumnunua mshambuliaji wa England, Harry Kane, ambaye ametimiza umri wa miaka 30 jana Ijumaa. (***Telegraph***)

### ...PSG NAO WAJITOSA

KLABU ya Paris St-Germain pia iko mguu sawa kumsajili Harry Kane iwapo Tottenham Hotspur wataamua kumuuza. (***Sky Sports***)

### AMRABAT ATAKIWA MAN

MANCHESTER United inaendelea na mazungumzo na Fiorentina kuhusu kiungo wa kati wa Morocco, Sofyan Amrabat mwenye umri wa miaka 26 kuziba nafasi ya Mbrazil Fred mwenye umri wa miaka 30, anayetarajiwa kuondoka katika klabu hiyo. (***90Min***)

### DYABALA KUBAKI ROMA

CHELSEA imepata pigo katika mbio zake za kumsajili mshambuliaji wa Argentina mwenye umri wa miaka, 29 Paulo Dybala ambaye anakaribia kusaini mkataba mpya na Roma. (***Tuttomercatoweb***)

### VERRATI ANAKARIBIA

KIUNGO wa kati wa Italia, Marco Verratti mwenye umri wa miaka 30 anakaribia kukamilisha uhamisho wake wa kwenda Al Hilal akitokea Paris St-Germain. (***Fabrizio Romano***)

### RAYA, DE GEA WAWINDWA

KLABU ya Bayern Munich inavutiwa na kipa wa Brentford, David Raya mwenye umri wa miaka 27 na David de Gea mwenye miaka 32, ambaye ni mchezaji huru baada ya kuondoka Manchester United. (***Times***)

### KUDUS AITAKA ARSENAL

KIUNGO wa kati wa Ajax na Ghana, Mohammed Kudus mwenye umri wa miaka 22, ameelezea mapenzi yake mkubwa ya kujiunga na Arsenal badala ya Chelsea. (***Football transfers***)

### CHELSEA YAKATALIWA

CHELSEA imekataliwa ofa yake ya pauni milioni 24 kwa ajili ya kumnunua mshambuliaji wa Montpellier, Elye Wahi mwenye umri wa miaka 20. (***Standard***)

### ROMEO LAVIA AFIKIRIWA

CHELSEA inafikiria kumnunua kiungo wa kati wa Southampton raia wa Ubelgiji, Romeo Lavia mwenye umri wa miaka 19 baada ya ofa yao ya pauni milioni 80 kwenda Brighton kwa ajili ya kiungo wa Ecuador Moises Caicedo kukataliwa. (***Athletic***)

### ODOI AWANIWA

KLABU ya Fulham imewasilisha ombi la kumnunua winga wa Chelsea, Callum Hudson-Odoi mwenye umri wa miaka 22 kwa ada ya pauni milioni 4. (***Fabrizio Romano)***

### JAMES KUTUA SAO PAULO

KIUNGO wa kati wa zamani wa Everton, James Rodriguez anakaribia kujiunga na klabu yake ya 10. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31 anakaribia kuhamia Sao Paulo kama mchezaji huru. (***Sun***)

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# REAL MADRID IMEKAMILIKA – ANCELOTTI

### Kocha huyo amesema hata kama wasipomsajili Mbappe msimu huu bado wanaweza....

**HOUSTON,** Marekani

CARLO Ancelotti amesema kuwa kikosi chake cha Real Madrid tayari "kimekamilika" ...hata bila kuongezwa kwa Kylian Mbappé -- baada ya ushindi wao wa mchezo wa kirafiki wa 2-0 dhidi ya Manchester United kule Houston nchini Marekani, juzi.

Jude Bellingham aliyewasili Madrid kwa kitita cha euro milioni 103 alifunga bao la kwanza mapema kwenye uwanja wa AT&T, kabla ya mchezaji mwingine aliyesajiliwa majira haya ya joto, Joselu kuongeza la pili.

Ancelotti amekuwa akisema mara kwa mara kwamba anafuraha na kikosi chake, licha ya kuondoka kwa mchezaji namba tisa Karim Benzema na viungo huku Mbappé, aliyezuiwa na Paris Saint-Germain akihusishwa kujiunga nao.

"Kikosi kiko sawa," alisema Ancelotti.

"Hatutakuwa na matatizo na kikosi. Kikosi ni kizuri. Kimekamilika."

Alipoulizwa kuhusu Mbappé, Muitaliano huyo alilikwepa swali ili na kukusitiza kikosi chake kimekamilika na kuomba kuulizwa swali lingine, alijibu; "Swali linalofuata."

Ushindi huo dhidi ya United unamaanisha kuwa Madrid wameshinda mechi zao zote mbili za kirafiki za kujiandaa na msimu mpya nchini Marekani hadi sasa, baada ya ushindi wa 3-2 dhidi ya AC Milan kwenye uwanja wa Rose Bowl huko Pasadena, California Jumapili.

Miamba hao wa Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga, wamewaongeza Bellingham, Joselu, Arda Guler, Fran Garcia na Brahim Diaz kwenye kikosi chao msimu huu wa joto.

"Bao la Bellingham limeonesha ubora alionao," aliongeza Ancelotti. "Anazidisha mbio zake kutoka kwa kina kirefu. Antonio Rudiger alimpa pasi nzuri na kufunga. Na la Joselu ni bao ambalo hulioni mara kwa mara."

Mbappé anafanya mazoezi na wachezaji wa akiba wa PSG baada ya kuachwa nje ya ziara yao ya Japan, huku klabu hiyo ya Ufaransa ikitaka kuweka shinikizo kwa fowadi huyo ama kuongeza mkataba wake zaidi ya msimu ujao wa joto, au kuhama sasa, badala ya kuondoka kwa uhamisho wa bure.

Huku Joselu akiwa ndiye fowadi pekee wa asili katika kikosi cha Madrid kwa sasa, Ancelotti amekuwa akijaribu mfumo mpya wa 4-4-2 akiwa na Vinicius Junior na Rodrygo Goes.

"Inaendelea vizuri," alisema. "Nadhani Vinicius anabadilika. Anapenda kucheza ndani zaidi kidogo... Rodrygo na Vinicius ni hatari sana wakiwa na mpira. Tunaweza kuwa moja kwa moja katika mabadiliko, na ubora wa Bellingham utasaidia hilo."

Madrid itacheza na Barcelona mjini Arlington, Texas leo Jumamosi, na kisha Juventus mjini Orlando, Florida Agosti 2, kabla ya kurejea kutoka Marekani.

## Silva astaafu soka akiwa na miaka 37

**BARCELONA,** Hispania

GWIJI wa Manchester City, David Silva ametangaza kustaafu kucheza soka akiwa na umri wa miaka 37, siku chache baada ya kuumia goti.

Silva alikuwa amepanga kuendelea na soka katika klabu ya Real Sociedad, lakini jeraha la goti alilolipata kabla ya msimu mpya limetishia kumweka nje kwa muda mwingi wa msimu ujao na kuamua kubadili mipango yake.

"Leo (jana) ni siku ya huzuni kwangu," alisema Silva katika ujumbe wa video uliotumwa kwenye mitandao ya kijamii.

"Leo (jana) ni wakati wa kuaga kile ambacho nimejitolea maisha yangu yote. Nitakumbuka sana. Asante kwa kunifanya nijisikie nyumbani."Silva alianza maisha yake ya soka kule Valencia, ambapo alicheza mechi 168 na kubeba kombe la Hispania, lakini ubora wake ulikuja City, ambao alijiunga nao mwaka 2010 na kuwa gwiji wa klabu.

Kiungo huyo mbunifu alikuwa sehemu muhimu ya timu ya City ambayo iliyonyanyua taji la kwanza la ligi kuu ya England msimu wa 2011-12 katika siku ya mwisho ya msimu.

Alishinda mataji mengine matatu ya ligi kuu akiwa na City, mawili ya mwisho akiwa chini ya kocha Pep Guardiola.

Silva amewekewa sanamu nje ya uwanja wa Etihad pamoja na wachezaji wenzake wa zamani Vincent Kompany na Sergio Aguero.

Silva aliondoka City mwaka 2020 baada ya kucheza mechi 436 na kurejea LaLiga katika klabu ya Sociedad.







# LAPORTA: MESSI KUCHEZA MAREKANI NI HISIA YA AJABU

**BARCELONA,** Hispania

RAIS wa Barcelona, Joan Laporta ameiambia ESPN ni "hisia ya ajabu" kumuona Lionel Messi akiwa na jezi ya Inter Miami CF, lakini anamtakia fowadi huyo kila la heri kwenye Ligi Kuu ya soka ya Marekani, MLS.

Messi mwenye umri wa miaka 36 aliondoka Barcelona na kwenda Paris Saint-Germain miaka miwili iliyopita, lakini timu hiyo ya Katalunya ilijaribu kumsajili tena mapema msimu huu wa joto wakati mkataba wake na timu hiyo ya Ufaransa ilipokwisha.

Timu ya Saudi Arabia Al-Hilal pia ilimpa Messi mkataba, lakini mchezaji huyo wa kimataifa wa Argentina aliamua kujiunga na Inter Miami, ambapo amefunga mabao matatu katika mechi zake mbili za kwanza.

"Ni hisia ngeni," Laporta aliiambia ESPN kuhusu kumtazama Messi akicheza Marekani.

"Tulimtambulisha Messi na Barcelona. Hivyo ndivyo ninavyofikiri mashabiki wengi wanamwona Messi, kwa sababu muda mwingi wa soka yake amekuwa Barca.

"Lakini tunaheshimu uamuzi wake na tunamtakia mema. Tunawatakia mema wachezaji wetu. Alikuja Barcelona akiwa mtoto, mwenye umri wa miaka 14, na alikaa nasi kwa miaka 20. Natumaini anaweza kuwa mzuri sana."

Messi tayari ameunganishwa Miami na wachezaji wenzake wa zamani wa Barca Sergio Busquets na Jordi Alba, huku Luis Suarez pia akihusishwa, ingawa vyanzo vimeiambia ESPN mshambuliaji huyo wa Uruguay atabakia Gremio hadi angalau mwisho wa mwaka.

Laporta alisema anaelewa uamuzi wa Messi kuchukua changamoto mpya nchini Marekani, hata kama Barca wangeondoa uwezekano wake wa kurejea LaLiga.

# Havertz hana uhakika kikosi cha kwanza

**LOS ANGELES,** Marekani

KAI Havertz, amesema hatarajii kuingia moja kwa moja kwenye kikosi cha kwanza cha Arsenal licha ya kuwa mchezaji wa tatu ghali zaidi katika historia ya klabu hiyo.

Arsenal ilimsajili mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24 kutoka Chelsea kwa mkataba ambao unaweza kufikia takribani pauni milioni 67.5, ikimaanisha ni Declan Rice pekee (pauni milioni 105 kutoka West Ham United) na Nicolas Pepe (pauni milioni 72 kutoka Lille) waliogharimu klabu hiyo fedha nyingi zaidi.

Havertz ameunda sehemu ya safu mpya ya wachezaji watatu pamoja na Rice na Martin Odegaard nyakati hizi za maandalizi ya msimu mpya.

"Nadhani kila mtu lazima apate nafasi yake katika timu," alisema Havertz.

"Unacheza unapofanya mazoezi vizuri na kucheza vizuri kwenye michezo, nadhani lazima pia nitoe kila kitu katika kila mchezo, ndivyo ninavyoingia kwenye timu, sio mimi tu, bali pia kila mchezaji.

"Kwa hakika ni mtindo tofauti kabisa wa soka kuliko tulivyocheza Chelsea. Nadhani ni mtindo ambao unanifaa sana. Bila shaka huwa inachukua muda kidogo kuzoea hilo tena."

Havertz alibadilisha nafasi mara kwa mara wakati wa ushindi wa 5-3 wa kirafiki dhidi ya Barcelona Jumatano kwenye uwanja wa SoFi huko Los Angeles -- akihamia ubavu wa kushoto na pia kupitia katikati.

Alifunga bao dhidi ya klabu hiyo ya Katalunya na anaamini kuwa nafasi mpya ya Namba 8 katika mfumo anaopendelea Mikel Arteta wa 4-3-3 unaweza kumsaidia kugundua upya kiwango chake bora baada ya kipindi cha mchanganyiko cha miaka mitatu kule Stamford Bridge.

Licha ya kufunga bao la ushindi katika fainali ya ligi ya mabingwa Ulaya mwaka 2021 dhidi ya Manchester City, alijitahidi kupata matokeo bora baada ya kujiunga na Bayer Leverkusen, akifunga mabao 19 pekee katika michezo 91 ingawa alikuwa akicheza kama mshambuliaji wa kati mara kwa mara.




"Ninafurahia sana, kucheza nafasi hiyo kama namba 8," alionGeza Havertz.

"Niko kwenye mpira zaidi, nimeunganishwa zaidi kwenye mchezo. Ninafurahia sana. Nadhani nina nafasi kubwa ya kuimarika katika michezo, bado nazoea mchezo na kila kitu. Hadi sasa inafanya kazi kabisa."

# SAKHO AJIVUNIA KUPITA SIMBA

**Na Abdallah Mataka**



NYOTA wa zamani wa klabu ya Simba raia wa Senegal, Pape Osmane Sakho, amesema kuichezea timu hiyo ni moja ya maamuzi bora aliyowai kuyafanya na anajivunia kupita kwenye klabu hiyo.

Akizungumza na kituo kimoja cha radio cha jijini Dare s Salaam, Sakho alisema kucheza Simba kumemfungulia milango mingi katika kupaa kisoka tangu aanze kucheza mchezo huo.

Alisema akiwa Simba ndipo alipoitwa kwa mara ya kwanza kwenye kikosi cha timu ya taifa ya wakubwa cha Senegal akiwa na nyota wengine wengi wanaocheza soka la kulipwa Ulaya.

"Mbali na kuitwa timu ya taifa, lakini pia Simba imenifungulia milango kucheza soka Ulaya, kwa kweli nilikuwa na wakati mzuri sana, Simba imenipa nafasi yakuonyesha kipaji changu na kuonekana, klabu hiyo na Tanzania kwa ujumla itaendelea kuwa moyoni mwangu," alisema Sakho.

Alisema mafanikio ya juu zaidi atakayoyapata kuanzia sasa Simba itakuwa na mchango wake.

**Alisema anawashukuru viongozi wa timu hiyo na wachezaji kwa ushirikiano waliompa muda wote akiwa ndani ya timu hiyo.**

"Kwa kiasi kikubwa ndoto zangu zinakamilika, ndoto ya kuona naitwa timu ya taifa, lakini kubwa zaidi ndoto ya kucheza soka ulaya, kazi niliyonayo ni kuendelea kupambana kwa kujituma zaidi ili niendelee kwenda mbele zaidi," alisema Sakho.

Mshindi huyo wa goli bora la michuano ya club bingwa barani Afrika mwaka 2022 amejiunga na timu ya US Queivelly Rouen inayoshiriki ligi daraja la kwanza nchini Ufaransa akitokea Simba.



Naibu Waziri, Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Hamis Mwinjuma 'Mwana FA' (kulia) akizungumza na mwakilishi wa La Liga nchini Tanzania, Jorge Gazapo kwa ajili ya kuangalia maeneo mbalimbali wanayoweza kushirikiana katika kuendeleza sekta ya michezo hapa nchini. **PICHA: BIN ZUBERY**

# Geita Gold FC yaitaka 'Top Four'

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA mpya wa Geita Gold FC, Hemed Suleiman 'Moroco' amesema lengo lake namba moja msimu ujao wa ligi kuu Tanzania bara ni kuhakikisha timu hiyo inamaliza katika nafasi nne za juu (Top Four).

Akizungumza kutoka Morogoro ambapo timu hiyo imeweka kambi kwa ajili ya maandalizi ya msimu ujao, kocha huyo aliyechukua nafasi ya Fred Felix Minziro aliyetimkia Prisons, amesema kwa usajili walioufanya na mazoezi ambayo amekuwa akiwapa wachezaji wake, ana imani kubwa ya kufikia lengo hilo.

"Nimeanza vizuri, wachezaji wanajaribu kuzoea kile ambacho ninawafundisha, nawashukuru wao na viongozi wa klabu hii pia, malengo yetu ni kuona msimu ujao tunafanya vizuri zaidi kuliko msimu uliopita, naamini kwa jinsi tulivyofanya usajili na wachezaji waliopo hapa kitu hicho kinawezekana kabisa," alisema Morocco.

Kikosi hicho kimepiga kambi Morogoro tangu Julai 19 kujiandaa na msimu mpya na inatarajia kumaliza Agosti mbili na kurejea mkoani Geita kwa maandalizi ya mwisho kabla ya kuanza kwa ligi kuu Tanzania Bara msimu wa 2023/24 Agosti 15.

Msimu uliomalizika Geita Gold ilimaliza ligi ikiwa nafasi ya saba ikivuna 37 na hivyo kushindwa kupata nafasi ya kushiriki michuano ya kimataifa kama ilivyokuwa msimu wa 2021/22.

Msimu wa 2021/22, Geita Gold ilimaliza nafasi ya nne ikiwa na pointi 46 na kukata tiketi ya kucheza michuano ya Kombe la Shirikisho barani Afrika ambapo ilitolewa na Hilal Al Sahil ya Sudan katika hatua za mwanzoni.

## Robertinho ajivunia fiziki wachezaji wake

INATOKA UK 24

Simba inatarajia kurejea nchini Agosti Mosi tayari kwa tamasha lake la 'Simba Day' ambalo kilele chake kitakuwa Agosti 6.

Simba itacheza mchezo wa kimataifa wa kirafiki siku hiyo ya kilele cha Simba Day na baada ya hapo inatarajia kuelekea jijini Tanga kwa ajili ya michezo ya Ngao ya Jamii.

Kikosi hicho cha Robertinho kitacheza na Singida Fountain Gate na mshindi wa mechi hiyo atacheza na mshindi wa mechi kati ya Yanga na Azam kupata timu mbili zitakazocheza mchezo wa mwisho kuwania Ngao ya Jamii kwa msimu mpya wa 2023/2024



## Yanga SC kutoidharau Asas

INATOKA UK 24

mapema kabla ya kufika huko walikoweka malengo yao.

"Tujifunze kwa watani zetu, mwaka 2019 na 2021 walitolewa na timu ambazo hawakutarajia, walitoka kufika hatua ya makundi lakini miaka hiyo wakaondolewa hatua ya kwanza kabisa, sisi hatutaki kupitia hayo," alisema Kamwe na kuongeza,

"Hii ni michuano ambayo kuna wakati ina matokeo ya kushangaza, lazima tuchukue tahadhari katika kila mchezo na hatua tunayopita," alisema.

Yanga itaanzia ugenini nchini Djibouti kati ya Agosti 18-20 dhidi ya timu hiyo kabla ya kuja kurudiana nayo jijini Dar es salaam kati ya Agosti 25-27.

Kama itafanikiwa kuwatupa nje Wadjibouti hao itakutana na mshindi wa mchezo kati ya AS Otoho na El Marreikh kuwania kutinga hatua ya makundi ya michuano hiyo,.

Uongozi wa Yanga umeweka wazi malengo yao ya kwanza ni kuhakikisha wanatinga hatua hiyo ya makundi.

Michezo
Nipashe
Jumamosi Julai 29, 2023



UK. 22

Silva astaafu soka akiwa na miaka 37



Kiungo wa Yanga, Stephan Aziz Ki akimiriki mpira wakati wa mazoezi ya timu hiyo yanayofanyika Avic Town nje kidogo ya jiji la Dar es salaam kwa ajili ya kujiandaa na msimu mpya wa ligi kuu 2023/2024 unaotarajiwa kuanza Agosti 15. **PICHA: MTANDAO**

# Robertinho ajivunia fiziki wachezaji wake

●●● Atamba 'zimwi' la majeruhi litapunguza kuwaandama wachezaji wake msimu ujao, kurejea nchini..

**Adam Fungamwango na Saada Akida**

WAKATI zikiwa zimebakia siku tatu kabla ya kuanza safari ya kurejea nchini kutoka Uturuki, Kocha wa Simba, Roberto Oliveira 'Robertinho' amesema ameridhishwa na utimamu wa mwili walionao wachezaji wake kwa sasa na hiyo itawasaidia kuepuka majeraha madogo madogo.

Roberthino, alisema siku tatu zilizobakia atazitumia kuongeza makali kwenye safu yake ya ushambuliaji ambayo msimu ujao itakuwa chini ya Luis Miquissone, Aubin Kramo, Willy Onana, Jean Baleke, Denis Kibu, Iddi Chilunda, Moses Phiri na nahodha John Bocco.

Akizungumza jana kabla ya mazoezi ya jioni, Robertinho alisema ameona wachezaji wake wengi wakiwa na utimilifu wa mwili na hii inampa matumaini ya kuwa na kikosi imara.

"Hii ni muhimu kwa sababu huko mbele hawatoweza kupata tena nafasi ya kuwajenga sana zaidi ya kuwarudishia tu ufiti unaopotea kwa sababu tutakuwa na mashindano mengi, nalipongeza benchi langu la ufundi upande wa mazoezi ya viungo, angalia kwa sasa sisikii habari ya wachezaji wenye matatizo ya misuli na hiki ni kitu kizuri sana na kitatusaidia mbele ya safari," alisema kocha huyo raia wa Brazil na kuongeza,

"Nimeridhika na kikosi changu pamoja na maandalizi yote tunayofanya kambini, nikwambie tu kwa sasa tuna vikosi viwili vyenye uwezo unaofanana," alisema kocha huyo uku akitoa pongezi kwa wasaidizi wake wa mazoezi ya viungo.

Jopo la makocha wa viungo la timu hiyo msimu huu linaongozwa na Corneille Hategekimana raia wa Rwanda.

Robertinho alisema kwa sasa anakamilisha program yake aliyokuwa ameiandaa kwa ajili ya kambi ya nchini humo na watarejea nchini wakiwa na kikosi imara.

INAENDELEA UK 23

## Yanga SC kutoidharau Asas kuhofia ya Jwaneng Galaxy, UD Song

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Yanga imesema haitoidharau kamwe klabu ya AS Ali Sabieh Telecom (ASAS) ya Djibouti ambayo imepangwa nayo mechi ya awali ya Ligi ya Mabingwa Afrika ili yasije kuwakuta kama yaliyowakuta watani zao Simba walipotolewa pasipo kutarajia na klabu ya UD Songo 2019, na Jwaneng Galaxy, 2021.

Ofisa habari wa klabu hiyo, Ali Kamwe, amesema jana kuwa hawatofanya kosa lolote la kuwadharau wapinzani hao kwa sababu kuna wakati Ligi ya Mabingwa Afrika kuwa na matokeo ya kushangaza.

Aliwatahadharisha baadhi ya wanachama na mashabiki wa timu hiyo ambao akili yao inawaaminisha kuwa Asas ni timu ndogo na kuiwaza zaidi El Merreikh ya Sudan ambao wanaweza wakacheza nao kama Wasudan hao watawatoa AS Otoho ya Congo Brazzaville.

"Ili kufikia malengo yetu ya mwanzo ya hatua ya makundi msimu huu ni lazima kwanza tushinde mechi yetu ya hatua ya awali dhidi ya ASAS, mechi ya kwanza Djibouti, ya pili hapa Dar es Salaam na hapa wanachama na mashabiki wa Yanga wanatakiwa wanielewe vizuri kabisa, nimeona mijadala ikianza eti tunarudi Sudan kucheza na El Merrikh sijui nini, hii tunakosea sana kwa sababu hata hao Wasudan wana mchezo dhidi ya Otoho, sasa ikitokea sisi akili yetu yote ikiwa inamuwaza Msudan akienda kutolewa na Wakongo Brazaville matokeo yake tunakutana na mpinzani ambaye hatukujiandaa naye," alisema Kamwe.

Aidha alisema kama akili yao ikiiwaza sana El Merreikh mechi ya raundi ya kwanza, basi watapunguza umakini kwenye mechi ya hatua ya awali na kuweza kutolewa

INAENDELEA UK 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002